# Nipashe

Ijumaa Januari 3 , 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580118

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Wafanyabiashara watulizwa hofu kuhusu jeneza lililokutwa sokoni

UKURASA 21


UCHUMI

Simulizi aliyepona kwa dawa asili, sasa muuzaji wake maarufu
Ukurasa 18

BUFE
Ijumaa Januari 3, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

HATIMAYE INAFUFULIWA... Neema msaada wa Japan kurejesha Tafico, mapya soko la samaki kitaifa
Ukurasa 14

WAPOKEA SALAMU ZA JPM
TARI YAJA NA MPANGO MKAKATI WA MBEGU BORA MAZAO KUFIKA TANZANIA YA VIWANDA
Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18
Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# Anaswa na mihuri 66 ya jeshi, benki, TRA

**IMO** pia ya ofisa biashara wilaya, watendaji mitaa, stika za bima, vyeti feki vya wanafunzi ...*Endelea ukurasa wa 2*



# SIMANZI
## VILIO VYATAWALA KESI KABENDERA

UKURASA 2

Erick Kabendera akilia baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, kumkatalia kwenda kumzika mama yake. **PICHA: MTANDAO**

# Nyumba za NSSF zagawiwa wanafunzi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store


**MICHEZO** SIMBA YAFUNGUKA ILIPOWAZIDI YANGA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi baada ya kuwajulia hali wagonjwa, katika Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Anaswa na mihuri 66 ya jeshi, benki, TRA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Abraham Obed (55), mkazi wa Kata ya Isanga jijini Mbeya, kwa tuhuma za kughushi mihuri 66 ya taasisi mbalimbali, likiwamo ya jeshi hilo, mahakama na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, alidai mtuhumiwa huyo alikamatwa Desemba 31, mwaka jana, majira ya saa 11 jioni katika Mtaa wa Sokoine, Kata ya Sisimba.

Alidai jeshi hilo lilipata taarifa za siri kutoka kwa baadhi ya wananchi jijini humo wakimtuhumu kughushi mihuri hiyo na kisha kuitumia kutengeneza nyaraka bandia kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Kamanda Matei alidai kwamba, baada ya kupata taarifa hizo, walianza uchunguzi na walipomkamata walimkuta na mihuri hiyo pamoja na baadhi ya nyaraka ambazo alikuwa amezitengeneza kwa kutumia mihuri hiyo.

Alizitaja taasisi zingine ambazo mtuhumiwa alighushi mihuri yake kuwa ni benki za NMB na Access Tawi la Mbeya, Ofisi ya Ofisa Biashara wa Wilaya ya Mbeya, wenyeviti wa mitaa mbalimbali pamoja na watendaji wa mitaa.

Alidai kuwa mbali na kukamatwa na mihuri hiyo, mtuhumiwa pia alikutwa na kompyuta mpakato moja, stika za bima na vyeti vya wanafunzi mbalimbali ambavyo ni vya kughushi.

"Awali mtuhumiwa huyu alikuwa Wakala wa Bima wa Kampuni GMT, lakini baadaye akasimamishwa kazi na aliposimamishwa, akaamua kujiingiza kwenye biashara hii haramu na hakutaka kwenda kulima," alidai.

Kamanda Matei alidai kuwa hivi karibuni baadhi ya walimu walikamatwa wakiwa na nyaraka feki kwa ajili ya kuombea mikopo benki na huenda mtu huyo alihusika katika utengenezaji wa nyaraka hizo.

Alisema kwa sasa wanaendelea kufanya uchunguzi ili kujua vitu vingine alivyokuwa anaghushi mtuhumiwa huyo na kwamba jeshi hilo linawasiliana na maofisa wa TRA, ili wakamuhoji mtuhumiwa kujua watu aliowauzia mihuri yenye nembo ya mamlaka hiyo nyeti.

Pia, alisema watashirikiana na taasisi mbalimbali kufanya tathmini ili kubaini hasara ambayo mtuhumiwa huyo ameisababishia serikali kutokana na kughushi mihuri hiyo pamoja na nyaraka.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alithibitisha kuwa watoto wawili wa familia moja; Faisal Mashaka (5) na Farhana Mashaka (mwaka mmoja na miezi mitano) waliokuwa wamepotea katika mazingira ya utata, wamepatikana mkoani Tabora.

Alisema jeshi hilo limeshatuma maofisa wake mkoani Tabora ambao wamefuatana na wazazi wa watoto hao kwenda kuwachukua.

Alisema amewasiliana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora ambaye amemthibitishia kuwa mtuhumiwa mmoja anashikiliwa kutokana na kuhusika na tukio hilo.


fcs
FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY

**UFAFANUZI JUU YA WITO ZA MAOMBI YA RUZUKU KUTEKELEZA MIRADI MWAKA 2020**

FCS inapenda kutoa ufafanuzi zaidi juu ya matangazo yetu mawili ya wito wa maombi ya ruzuku yaliyotoka **tarehe 23/12/2019** katika Magazeti ya **Nipashe na Mwananchi** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika mwaka 2020, kama ifuatavyo:

a. **Ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuimarisha ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020** ***(Hili ni Mahususi kwa ajili ya Taasisi za Watu wenye Ulemavu Tu – Disabled People Organizations)***

b. **Ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa Mashirikika Yasiyo ya Kiserikali Zanzibar kwa mwaka 2020** ***(Hili ni Mahususi kwa ajili ya Taasisi na mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Zanzibar (Unguja na Pemba) tu.***

Kwa mantiki hiyo ruzuku hizi ni maalum. Taasisi ambazo si za watu wenye ulemavu (DPOs) na ambazo si za Zanzibar hazihusiki na ruzuku hizi. Taasisi zote ambazo zinakidhi vigezo kulingana na wito wa maombi uliotolewa, ikiwa ni pamoja na zile zenye ufadhili toka FCS na zinazoendelea kutekeleza miradi kwa sasa zinaruhusiwa kuomba.
Tarehe ya Mwisho ya kutuma maombi ni **31 Januari, 2020 Saa 10.30 Jioni.** Maombi yanaweza kutumwa kwa rejesta ama kuletwa ofisini kwa mkono. FCS haitapokea maombi yatakayotumwa kwa njia ya Kielektroniki. Ofisi za FCS itafunguliwa Tarehe 8 Januari 2020 saa 02: 30 Asubuhi, maombi yataanza kupokelewa kuanzia tarehe hiyo mpaka tarehe ya mwisho iliyotajwa hapo juu.
**FOMU ZOTE ZA MAOMBI ZINAPATIKANA KATIKA TOVUTI YA FCS http://thefoundation.or.tz/grants-applications/**

**Kwa maelezo zaidi fika ofisi za Foundation for Civil Society zilizopo**

**7 Madai Crescent, Ada Estate**
**Plot No. 154**
**Simu: +255 22 2664890-2**
**Baruapepe: information@thefoundation-tz.org**
**Tovuti: www.thefoundation.or.tz**

61557I202


# Vilio, simanzi vyatawala kesi ya Kabendera

**Na Hellen Mwango**

VILIO na simanzi vilitawala jana katika ukumbi namba moja wa Mahakaka ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya wanaodaiwa kuwa ndugu na marafiki wa mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, kufikishwa kwa ajili ya kusikiliza kesi yake.

Kabendera anadaiwa kupanga na kushirikiana na genge la uhalifu na shtaka la tatu ni la kukwepa kodi zaidi ya Sh. milioni 173.

Wakati mahakama ikisubiriwa kuanza shughuli zake katika ukumbi huo, Nipashe ilishuhudia mshtakiwa huyo akivua miwani na kukufuta machozi, huku wanaodaiwa kuwa ndugu zake wakisikika wakilia na sauti za chini.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Janeth Mtega, ilianza shughuli zake saa 6:33 mchana, huku upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi Lenatus Mkude na Wankyo Simon.

Mkude alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba mshtakiwa aliwasilisha maombi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) chini ya kifungu cha 194 (A) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20.

Alidai kuwa maombi hayo ya Desemba 18, mwaka jana, yalipokelewa na kulikuwa na vitu vya kurekebisha kupitia mawakili wa utetezi, lakini mazungumzo bado yanaendelea, hivyo Jamhuri kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

### AGONGA MWAMBA KUMZIKA MAMA

Wakili wa utetezi, Jebra Kambole, aliwasilisha maombi mahakamani hapo kwamba Kabendera amefiwa na mama yake mzazi, hivyo wanaiomba imruhusu kwenda Bukoba mkoani Kagera kuhudhuria mazishi au kutoa kibali cha kutoka mahabusu kwenda Kanisa Katoliki Chang'ombe, Temeke, jijini Dar es Salaam kutoa heshima za mwisho.

Alidai kuwa ibada ya kusalia mwili wa marehemu mama wa mshtakiwa huyo

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Gari la kampuni inayojenga barabara ya Ocean Road jijini Dar es Salaam likimwaga maji kupunguza vumbi ili kuweka mazingira bora ya kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usafiri wakwamisha kesi ya vigogo IPTL

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imeambiwa na Upande wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili wafanyabiashara Harbinder Sethi, James Rugemalira na Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni ya Kufua Umeme (IPTL), Joseph Makandege, kwamba wameshindwa kufikishwa mahakamani kutokana na tatizo la usafiri kwa Jeshi la Magereza.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini kutokana na tatizo la usafiri, watuhumiwa hawajafikishwa mahakamani, hivyo Upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 13, mwaka huu.

Mnamo Desemba 20 mwaka jana, Upande wa Jamhuri ilimuunganisha Makendege ambaye ni wakili wa kujitegemea na wafanyabiashara hao katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi na kutakatisha jumla ya Dola za Marekani 980,000.

Makandege amefanya idadi ya washtakiwa katika kesi hiyo kufikia watatu na idadi ya mashtaka kufikia 15 kutoka 12 ya awali.

Kigogo huyo alisomewa mashtaka matano ya kula njama, kuratibu genge la uhalifu, kujipatia na kutakatisha fedha, mbele ya Hakimu Mkazi Thomas Simba.

Jopo la Upande wa Jamhuri linaongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Paul Kadushi, Faraja Nchimbi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

INAENDELEA UK. 8

# Nyumba NSSF zageuzwa hosteli

**Na Mwandishi Wetu**

VYUO vikuu vinne na taasisi moja jijini Dar es Salaam, vimeingia makubaliano ya kupangisha nyumba za Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) za Mtoni Kijichi jijini kwa ajili ya malazi ya wanafunzi 17,820.

Vyuo hivyo ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (Duce), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT) na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).

Makubaliano baina ya NSSF na vyuo hivyo yalifikiwa hivi karibuni kwa kutia saini mkataba maalumu utakaowezesha wanafunzi kutumia nyumba hizo kama hosteli.

Akizungumza wakati wa kutia saini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Willium Erio, alisema uamuzi huo utawawezesha wanafunzi kuishi maeneo mazuri na salama.

Alieleza namna mgawanyo wa wanafunzi kwa kila chuo kuwa ni Duce (3,000), IFM (3,500), DIT (320), TIA (5,000) na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (6,000).

"Tumesaini makubaliano ya awali ambayo ni muhimu kwa pande zote mbili, kwetu (NSSF) wakati tunakamilisha taratibu za kuwapangisha, tunajua soko likoje na wao wanakuwa na uhakika kwamba wanaenda kuzungumza na wanafunzi kuwaeleza kuhusu makazi haya," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, eneo la Mtoni Kijichi kuna nyumba ambazo zipo tayari kwa ajili ya kutumika, ambazo zinaweza kuchukua wanafunzi 4,000.

Kaimu Mkuu wa Duce, Profesa Stephen Maluka, aliipongeza serikali kwa kuvifikiria vyuo kupata nafasi za makazi, akieleza kuwa chuo chake kina wanafunzi 6,000, lakini uwezo wake ni kuwapa malazi wanafunzi 420.

Naibu Mkuu wa IFM (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Emmanuel Mnzava, alisema wanaishukuru NSSF kwa kuwapatia fursa wanafunzi wao kukaa katika nyumba hizo.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MNADA WA FORODHA KWA NJIA YA MTANDAO

**Dar es Salaam, Januari 2, 2020:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi wote kuwa, kwa mara ya kwanza, mnada wa forodha kwa njia ya mtandao utafanyika tarehe 2 hadi 6 Januari, 2020 kupitia Tovuti ya TRA ambayo ni www.tra.go.tz.

Mnada huo utaanza saa 6:00 usiku tarehe 2 na kumalizika saa 5:59 usiku tarehe 6 Januari, 2020 ambapo washindi watatangazwa tarehe 7 Januari, 2020 kupitia tovuti ya TRA.

Ili kushiriki mnada huo kwa njia ya mtandao, mwananchi anatakiwa: -

1. Awe na kifaa kilichounganishwa na mtandao, kama vile Simu ya mkononi, Kompyuta ya mezani, Kompyuta mpakato yaani laptop n.k;
2. Awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi yaani TIN na kama hana TIN atatakiwa kujisajili kupitia tovuti ya TRA ya **www.tra.go.tz** ili kupata TIN kwanza;
3. Awe na barua pepe yaani ***email address;***
4. Awe na namba ya simu;
5. Awe amejisajili kwenye tovuti ya TRA kupitia ukurasa wa mnada kwa kubonyeza sehemu ya juu iliyoandikwa ***Auctions;***
6. Wakati wa kujisajili, mshiriki atahitajika kuhakiki kama jina alilojisajili limeshatumika na mtu mwingine ama la kwa kubonyeza kitufe cha tafuta **(Search icon)**. Hata hivyo, mtu yeyote anaweza kuona bidhaa zilizotangazwa kupitia mtandao hata kama hajajisajili;
7. Baada ya kujisajili, mshiriki ataweza kushindana na washiriki wengine kwa kuweka bei na atakuwa na uwezo wa kuongeza bei kadri ushindani utakavyokuwa ukiendelea;
8. Mshindi atapata ankara ya malipo ya awali ya asilimia 25 na ankara ya malipo ya kumalizia ya asilimia 75 kupitia mtandao na atakwenda benki kwa ajili ya kulipia;
9. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia 25 mara baada ya kupata ankara ya malipo wakati ankara nyingine ya malipo ya asilimia 75 atatakiwa kulipia ndani ya saa 48 ingawa kwa chombo cha moto kama vile gari, pikipiki n.k kutakuwa na ankara nyingine kwa ajili ya kulipia ada ya usajili; na
10. Baada ya kukamilisha malipo, mshindi atatakiwa kufika eneo la forodha mzigo ulipo kwa ajili ya kuchukua mzigo wake akiwa na uthibitisho wa kuonyesha kuwa yeye ndiye mnunuzi halali.

Kupitia taarifa hii, wananchi wote walioko ndani na nje ya nchi wanakaribishwa kushiriki mnada huo wa forodha kwa njia ya mtandao wenye haki sawa kwa kila mtu atakayeshiriki mnada.

Kwa maelezo zaidi, mwananchi anaweza kupiga simu katika Kituo cha Huduma kwa Mlipakodi kwa namba za bure **0800 75 00 75 au 0800 78 00 78.** Pia, anaweza kutuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp namba **0744 23 33 33** au kutuma barua pepe kwenda: **huduma@tra.go.tz.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**Richard Kayombo**

**Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**

215571902

# Adaiwa kuanzisha kiwanda bubu uchenjuaji wa madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kumkamata na kumhoji Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bunango, Kata ya Bugalama, Halmashauri ya Msalala, Kanjanja Kanjanja, baada ya kutuhumiwa kushirikiana na watoroshaji wa madini ya dhahabu. Inadaiwa watoroshaji hao wa madini wamefungua kiwanda bubu vya uchenjuaji wa madini katika halmashauri hiyo.

Biteko alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara ya kushtukiza katika nyumba iliyoko kijijini huko na kubaini uwapo wa kiwanda bubu cha uchenjuaji wa madini, ambacho kilianza uzalishaji tangu Julai mwaka jana.

Alidai ofisa mtendaji huyo amekuwa akipewa taarifa juu ya kiwanda hicho na mwenyekiti wa kijiji, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa, hivyo anapaswa kukamatwa na kuhojiwa kuhusu kiwanda hicho.

Biteko alisema serikali imekuwa ikiboresha sekta ya madini kwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini wilayani Kahama, lakini bado kuna baadhi yao wamekuwa wakiibia mapato kwa kuanzisha viwanda bubu kwenye makazi yao watu.

"Kiwanda hiki kipo hapa katika nyumba hii tangu Julai mwaka jana, huku kikiendelea kufanya kazi, serikali imepoteza mapato mengi kwa kutochukua hatua za haraka, tutachukua hatua kali za kisheria kwa mmliki wa mtambo huu na nyumba hii," alisema.

Waziri huyo aliwataka viongozi wa vijiji na mitaa wilayani humo kuhakikisha wanawafichua wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara haramu ya madini.

Biteko pia aliwaagiza viongozi wa Mkoa wa Shinyanga kudhibiti vitendo vya biashara haramu ya madini vinavyoendelea kushamiri katika maeneo mbalimbali, akibainisha kuwa mpaka sasa wameshanasa viwanda bubu viwili vya uchenjuaji wa dhahabu mkoani humo.

Katika ziara yake hiyo, Waziri Biteko pia alikamata mifuko 35 ikiwa na kemikali za uchenjuaji wa dhahabu katika kiwanda hicho, huku mashine yenye uwezo wa kubeba kilo 500 za Cabon ikiwa tayari imewekewa mzigo kwa ajili ya kuanza uchenjuaji.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akiondoa kipazia kuashiria kuweka jiwe la msingi la mradi wa miundombinu ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji katika eneo la Kinyasini Kisongoni, kulia ni Meneja Mradi wa Kampuni ya Kolon, Cho Kwang Lae. Hafla hiyo iliyofanyika Kinyasini Kisongoni Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, ikiwa ni shamrashamra za sherehe za Maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## Mbunge aona fursa kwa vijana utaliii

**Na Mwandishi Wetu,** BUSEGA

MBUNGE wa Busega mkoani Simiyu, Dk. Rafael Chegeni, amewataka vijana kuchangamkia fursa za kiuchumi zitokanazo na utalii kupitia tamasha la kukuza na kuendeleza utalii wilayani Busega la 'Lamadi Utalii Festival' lililofanyika kwa siku nne mjini Lamadi.

Akizungumza katika kilele cha tamasha hilo, Dk. Chegeni alisema vijana wengi wako mitaani bila kujishughulisha na miradi ya maendeleo, hivyo wakati sasa kuanza kubuni vitu mbalimbali vitokanavyo na fursa katika utalii.

"Huu ni mwanzo tu. Tamasha la Lamadi Utalii liwe chachu kwenu. Mji utakua kwa kasi zaidi kama miji mingine ya kitalii kama ilivyo Karatu, hivyo mchangamkie fursa na nyie hapa Lamadi.

"Muanze kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali ili hata watalii wanaoweza kuja hapa wavione na kuvinunua, wakinunua namna hii, mtapata kipato. Kwa hiyo, wito wangu kwa vijana wote sasa siyo muda wa kulala, ni muda wa kuchapa kazi," alisema.

Dk. Chegeni kupitia ofisi yake ya mbunge, aliahidi kutoa kiasi cha Sh. 500,000 ili kusaidia mafunzo kwa vijana wote watakaopenda kujifunza kuongoza watalii kwa muda mfupi.

"Naomba vijana mchangamkie fursa. Hapa tunae mtaalamu wa kuongoza watalii Nelson Machibya. Naomba ajitolee kuwasaidia na yupo tayari kwa hilo, lakini mimi natoa shilingi laki tano (500,000) za kufanikisha hilo," alisema.

Mbunge huyo pia alitumia nafasi hiyo kuwaomba wadau wa maendeleo kwenda Lamadi kuwekeza katika vyuo na shule za mambo ya utalii ili kuongeza fursa zaidi.

"Lakini kama itawezekana watu wachangamkie fursa kuja kuwekeza mafunzo ya kutembeza watalii. Watu wachangamkie hilo na tupo tayari kuwasaidia, mji bado una maeneo makubwa ya fursa," alitamba.

# Mwanafunzi mwaminifu alivyoshangaza

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA ulidhani vijana wema katika Jiji la Dar es Salaam wamekwisha, basi ulikuwa unakosea! Kwanini?

Katika hali isiyo ya kawaida kwa vijana wa jiji hilo ambao katika baadhi ya mitaa hupaswi kuwaamini, Elihuruma Patrick (22) (pichani), amedhihirisha vijana wema bado wapo jijini.

Iko hivi; mwanafunzi wa mwaka wa pili katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), juzi aliokota simu ya gharama kubwa ya mwandishi wa Nipashe, Juster Prudence, na ameirejesha kwenye ofisi za gazeti hili Mikocheni jijini.

Mwanafunzi huyo aliyeokota simu na mali zingine za Juster kwenye Kituo cha Daladala cha Mawasiliano, jana alifika ofisi za Nipashe na kukabidhi mali hizo.

Mali zenyewe ni simu aina ya Iphone, kadi ya benki na 'note book', ambayo mwandishi Juster alividondosha kituoni hapo.

Patrick (pichani) alieleza kuwa baada ya kuokota vitu hivyo alikwenda navyo hadi nyumbani na alipokagua 'note book', aliona namba za simu za Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Salome Kitomari, na akampigia simu kumjulisha kuwa ameokota mali hizo.

Baada ya kukabidhi mali hizo, Patrick alisema aliingiwa huruma na kuamua kuvipeleka vitu hivyo kwa Mwandishi Juster aliyedai alikaa naye kituo hicho cha daladala kwa muda wakisubiri basi.

"Alivyofika kabla hajakaa alinisalimia kiungwana na ndipo akakaa, alivyodondosha mali zake, nami nikaziokota zikiwa kwenye bahasha nikaona kuna simu na kadi ya benki ndipo niliamua kutafuta mawasiliano ya mtu wa karibu," alisema. "Nilikagua 'notebook' na kuna namba ya simu ya kwanza nikaipiga haikupatikana, nikaangalia upande mwingine nikakuta namba ya Kitomari ambaye ilipatikana na akanielekeza ofisi zilipo hadi nikafika," alieleza.

Uongozi wa Gazeti la Nipashe ulimpongeza mwanafunzi huyo kwa uaminifu mkubwa alioonyesha kwa kuikabidhi simu hiyo ya gharama kubwa.

"Dunia ya sasa waaminifu kama kijana huyu ni wachache sana, hii simu thamani yake ni kubwa, huyu kijana angeweza kuipeleka kwa mafundi wakaifanya kuwa yake na akaiuza na kupata fedha za kutumia, lakini amehakikisha anamtafuta mwenye nayo na kuileta, huu ni uaminifu mkubwa sana," Epson Luhwago, mmoja wa wahariri wa Nipashe, alisema.



## TANGAZO


game
Tsh16000 DEALS
NOW AVAILABLE AT GAME TANZANIA
DEALS VALID FROM 01 JANUARY UNTIL 31 MARCH
1 FOR Tsh16 000
Uht Full Cream Milk
26 FOR Tsh16 000
Apollo Noodles Packet
25 FOR Tsh16 000
Alpenliebe Candy 36g, Assorted
4 FOR Tsh16 000
Palm Oil 900Ml
2 FOR Tsh16 000
Weetabix Cereal 450g
40 FOR Tsh16 000
Dasani Still Water 500Ml
6 FOR Tsh16 000
Desperados Tequila Beer Bottles
2 PACKS FOR Tsh16 000
Always Home 3Piece Mug
2 FOR Tsh16 000
Big Jim 25L Storage Box
8 FOR Tsh16 000
Safari Lager 500Ml Can Beer
Tsh16 000 EACH
Sandisk Cruzer Glide 32Gb Usb
ANY 2 FOR Tsh16 000
Game 2Ply Soccer Ball Or Club Championship Tennis Ball
10 FOR Tsh16 000
Johnsons Baby Assorted Soap 100G
you've got game
View this catalogue online at www.game.co.tz
www.facebook.com/GameStoresTanzania
Game is committed to offer you the best service with the lowest price. In the unlikely event that you find the same product advertised by a competitor at a lower price, we guarantee to beat that price! . T's & C's apply.
DEALS VALID 01 JANUARY - 31 MARCH 2020 | 14325
ITEMS AVAILABLE WHILE STOCKS LAST
All prices listed are in Tanzanian shillings . All prices include VAT.
SHOPPING HOURS
• Monday - Sunday - 09h00 to 20h00
• Public Holidays - 09h00 to 20h00
TANZANIA, DAR ES SALAAM
Plot 2, Sam Nujoma Road
Telephone: (00255) 2197800 / 2221-97800
Massdiscounters reserve the right to control quantities of any item offered for sale. All prices, illustrations and copy are correct at the time of going to press, however, Massdiscounters cannot be held responsible for any changes or print errors that may occur. Prices exclude accessories used for advertising purposes.
Errors and omissions excepted.
Walmart Save money. Live better.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Hongera Kigwangalla kumalizana tofauti*

**MIONGONI** mwa habari zilizotikisa nchi katika kufunga mwaka 2019 na kuingia mwaka 2020 ni juu ya tofauti kati ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla na Katibu Mkuu wake, Prof. Adolf Mkenda.

Taarifa ya kutokupatana kwa viongozi hao wakuu wa wizara hiyo, ziliibuliwa na Rais John Magufuli alipofanya ziara Desemba 31, mwaka jana, katika Hifadhi ya Msitu wa Rubondo na kuzungumza na maofisa na askari wanyamapori.

Katika maelezo yake, Rais Magufuli alisema anasikitishwa na uhusiano mbaya baina ya viongozi hao, ambao kwa kiasi kikubwa ulisababisha baadhi ya shughuli katika wizara kuzorota.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa amekuwa akifuatilia utendaji kazi wa Dk. Kigwangala na Prof. Mkenda ambao umekuwa si wa kuridhisha kutokana na kugombana kwao.

Ugomvi wao huo, alisema umemfanya amwagize Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, awaite na kuwaeleza. Bila kuuma maneno, Rais magufuli alisema wateule wake hao wawili wamekuwa wakigombana kila uchao na kusababisha kazi za wizara kwenda arijojo.

Kutokana na tofauti hizo, aliweka wazi kwamba anawapa siku tano kuanzia Desemba 31, mwaka jana, wamalize tofauti zao, vinginevyo atatumia mamlaka aliyo nayo kutengua uteuzi wao.

Wakati umma ukisubiri kuona tofauti hizo zinazikwa na kulisukuma gurudumu la maendeleo kwa sekta wanazoziongoza, Dk. Kigwangalla juzi aliandika katika ukurasa wake wa Twitter kuwa wamepatana na kuwa kitu kimoja.

Kigwangalla katika ukurasa wake huo, alitanabahisha kuwa baada ya kikao chao na Katibu Mkuu Kiongozi, wamezika tofauti zao na sasa hali ni shwari.


Hizo ni habari njema kwa sababu kupatana kwao ni ishara kuwa wametii maagizo ya Rais kuwa wamalize tofauti zao ili kuiendeleza wizara hiyo ambayo imebeba moja ya sekta nyeti katika kutoa mchango kwenye pato la taifa.

Hatua ya kumaliza tofauti kati ya Dk. Kigwangalla na Prof. Mkenda licha ya kuonyesha ukomavu kutokana na hadhi zao za kielimu, pia kumeonyesha kuwa wal hali ya juu na kuleta imani kwamba sasa watafanya kazi kwa ushirikiano na maelewano.

Pamoja na hatua waliyoifikia, kama alivyosema Dk. Kigwangalla, ni vyema ikawa ya kweli badala ya kuwapaka Watanzania kwa mgongo wa chupa au kiutimiza msemo kwamba "funika kombe mwanaharamu apite". Wawili hao wanajenga nyumba moja, kwa nini kugombea fito?

Mapatano hayo yawe ya dhati na ni imani ya Watanzania kwamba yatakuwa ya kweli na kama yatakuwa ya unafiki, Rais Magufuli, kama alivyosema ana vyombo vya kufuatilia, atabaini kama si ya kweli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# *Tasaf iimulike kaya hii maskini bado inateseka*

Na Beatrice Moses

**MPANGO** wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), unaotekelezwa chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, unatajwa unalenga kuzifikia jumla ya kaya milioni 1.2, ambazo ni wastani wa watu milioni sita wanaoishi katika hali ya umaskini kwa Tanzania Bara na Visiwani.

Kuna vigezo vilivyowekwa kuzibaini na kuziorodhesha kaya hizo maskini, ili chini yake mkakati wa uhawilishaji fedha, zijengewe uwezo wa kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Hata hivyo, kuna haja ya kumulika vigezo vinavyotumika katika kubaini kaya hizo, kutokana na ukweli kwamba kuna dai la 'figisu' zinazosababisha mateso kwa walengwa.

Rais Dk. John Magufuli, kuna wakati alinyooshea vidole dhidi ya ufanisi kwenye mfuko huo, baada ya kubainika kashfa ya kaya hewa nyingi sana.

Ni vitendo vya baadhi ya watendaji wa serikali, hivyo ni wazi mfuko huo unapaswa kumulikwa kwa kila mara ili wanufaika wabaki kuwa walengwa.

Vivyo hivyo, kuna malalamiko kadhaa yamekuwa yakiibuka kutoka kwa baadhi ya kaya maskini kuenguliwa kwa vigezo visivyoainishwa vyema na Tasaf.

Kaya ya Abdallah Rashidi, inaweza kuingia katika orodha ya walalamikaji walioenguliwa kwenye mpango huo, hali inayosababisha wawe katika maisha magumu kiasi cha kushindwa kumwezesha mtoto wao mlemavu kupata huduma za matibabu.

Sakina Sadick, ni mama mzazi wa mtoto huyo, anayebainisha kuwa yuko katika wakati mgumu kumhudumia mtoto wao, Munira Rashid (12), sababu kuu ni pengo katika kipato chao.

Mtoto huyo ni mlemavu wa viungo, anayeishi na wazazi wake Saranga, wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam. Ni miaka miwili imepita tangu alipotakiwa kupimwa kichwa kwa kipimo cha CT- Scan, ikiwa ni hatua za awali kumsaidia kutibu tatizo ya kutoona alilolipata baada ya kuugua homa kali akiwa na umri wa miaka 9.

Mama huyo anawaomba wasamaria wema wajitokeze kumsaidia mtoto apate huduma ya tiba ya kipimo hicho, ili atibiwe macho, kwani analalama kusota tangu alipoandikiwa apimwe katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, wamekwama gharama za malipo. Sakina anabainisha kuwa awali walijitahidi kutafuta fedha hizo ambazo zilikuwa ni Sh. 160,000 wakapata nusu yake, (Sh. 80,000) ambazo baada ya muda, walijikuta wanazitumia kwa mahitaji mengine, pindi walipokwama kupata za kuongezea.

"Mwanangu Mnira nilimzaa mwaka 2008 akiwa mzima, lakini baada ya miezi minne ndipo nikabaini jambo tofauti mwilini mwake, kichwa kilianza kuwa kikubwa kwa kasi, tukampeleka CCBRT ambako alitibiwa na kufanyiwa upasuaji mara mbili, lakini hakurejea katika hali ya kawaida.

Anasema, Munira awali alikuwa anaona, lakini alipopatwa na homa kali akiwa na umri wa miaka 9, alilazwa katika Hospitali ya Mwananyamala, na baada ya hapo alianza kupoteza uwezo wa kuona na ndio imekuwa hali yake hadi sasa.

Ni hatua ndio inayoleta hitaji ya CT-Scan kwa ajili ya uchunguzi utakaomwezesha atibiwe. Mzazi huyo anasema, walishawahi kujiandikisha kutaka kuwa wanufaika wa Tasaf, lakini hawakukubaliwa.

Munira ni mtoto mwenye uwezo mzuri wa kujieleza na anasema, tamanio lake ni aende shule kusoma, lakini hawezi kutembea na alijifunza kuhesabu kwa kutumia 'visoda' nyumbani kwao.

Rashid Abdallah, baba mzazi wa mtoto huyo, anasema awali alikuwa akifanya kazi kwenye kituo cha mafuta, lakini alipunguzwa, hivyo amekuwa akitafuta kipato cha familia kwa kufanya vibarua, ikiwamo kusaidia mafundi kwenye ujenzi.

Anasema, Munira kwa sasa ni mkubwa na inakuwa kazi nzito kumbeba, hivyo anaamini iwapo watasaidiwa baiskeli, itawarahishia kumhudumia. Ombi lake ni wanajamii wamsaidie kwa kuwasiliana naye kwa namba ya simu: 0654728106.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga Godwin Muro, anakiri na kuunga mkono hitaji la kaya hiyo kupatiwa msaada, akibainisha kuwa aliwaandikisha kuwa wahitaji wa Tasaf, lakini cha kushangaza, jina liliondolewa, kwa majibu wanasaidiwa watoto wanaosoma.

Kwa hali inayoikabili familia hiyo, ni wazi kuna haja ya mtu mmoja mmoja au kikundi, hata ofisi za kiserikali zijitokeze kuwasaidia, maana ninarejesha imani kwamba Tasaf wakati wote iko kwa ajili ya maslahi ya umma.

Ni jambo linalotia moyo kwamba zipo kaya kadhaa tayari zimeshanufaika kupitia mpango huo, kupitia kuungwa mkono na serikali, katika kuhakikisha unasimamiwa vyema kufanikisha malengo.

Zipo kaya kadhaa masikini zimeshatoa shuhuda za jinsi ruzuku hizo zilivyowapunguzia umaskini wa kipato na kuwawezeshwa kupata huduma na mahitaji muhimu, ikiwamo malipo ya ada za shule, huduma za afya na kuboresha makazi yao.

## HABARI KITAIFA

# CCM yaahidi kufanya siasa kistaarabu uchaguzi 2020



**Restuta Damian,** BUKOBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimepanga kufanya siasa safi kwa mwaka huu ili kuendelea kuaminiwa na wananchi kwa kusikiliza na kuheshimu uamuzi wa umma huo.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (pichani), wakati akizungumza na viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya shina hadi wilaya na watumishi wa serikali mjini Bukoba wakati akitoa salamu za mwaka mpya.

Bashiru alisema uchaguzi wa mwaka huu utakuwa wa amani na utulivu kwa kuwa tayari chama kimejipanga kudhibiti mambo ambayo yanaweza kuondoa uvunjifu wa amani na unaoweza kuondoa usalama wa nchi.

"Kinachotakiwa katika siasa safi ni kuangalia amani na utulivu na chama kuanzia kwenu wanachama mjipange kudhibiti mambo ambayo yanaweza kuondoa amani ya nchi. Lengo letu tuwe na siasa safi," alisema Bashiru.

Alisema njia mojawapo ya kufanya siasa safi ni kuwa karibu na umma kwa kuonyesha kuvumiliana ndani ya chama hicho kwa kutovuka mipaka kwa kuwa kufanya hivyo ni kuleta aibu katika chama.

"Siasa safi ni kuwa karibu na umma kwa kwa ushiriki wa aina yoyote, kuvumiliana nyie kwa nyie bila kuvuka mipaka, hivyo itawaondolea aibu ya chama na kufanya upatikajaji wa siasa safi na yenye utulivu," alisema Bashiru.

Aidha, alisema endapo viongozi hawatafanya siasa safi, watasababisha viashiria vya uhujumu na kuweka nia ya kusimamia misingi ya kuongoza watu.

Dk. Bashiru aliongeza kuwa siasa hizo zizingatie kuwa na nafasi za wanawake bila kuwapatia vitisho wala udhalilishaji wa aina ya ugombea na kuwapiga fitina.

Alisema wanawake wana uwezo mkubwa wa kuongoza kada zozote katika chama, kwa kuwaamini kwa utendaji wao katika jamii ambazo wanatoa huduma za makuzi, malezi kwa kila hali hivyo chama hakitavumilia unyanyasaji katika uchaguzi.

## Bosi wa CRDB aahidi huduma bora zaidi

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, amesema benki hiyo imejipanga kuendelea kutoa huduma bora zaidi za kifedha nchi mwaka huu.

Bosi huyo alitoa ahadi hiyo, jana, alipotembelea na kupata huduma kwa wakala wa CRDB mjini Bukoba mkoani Kagera.

Akizungumza baada ya kupata huduma kwa wakala huyo, Nsekela aliwaomba wateja wa CRDB kuiamini benki hiyo na kuendelea kupata huduma kupitia mawakala wake waliozagaa nchi nzima.

"Niendelee kuwasihi wateja wetu kuwaamini na kuwatumia mawakala wa CRDB kwani wanatoa huduma zote kama benki, pia wapo karibu zaidi na makazi na maeneo ya biashara ya wateja wetu, hivyo kuwapunguzia gharama za usafiri kufuata huduma na hata muda.

"Mwaka jana tulifanikiwa kuongeza idadi ya mawakala wetu kutoka 5,000 hadi 12,000, ili kuhakikisha kuwa huduma zetu zinasogea karibu zaidi na wateja wetu," alisema.

Benki hiyo pia imekuwa ikishirikiana na serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tayari uongozi wa benki umeshatoa fedha kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge.

**"Niendelee kuwasihi wateja wetu kuwaamini na kuwatumia mawakala wa CRDB kwani wanatoa huduma zote kama benki, pia wapo karibu zaidi na makazi na maeneo ya biashara ya wateja wetu, hivyo kuwapunguzia gharama za usafiri kufuata huduma na hata muda.**




HABARI KITAIFA

# Vilio, simanzi vyatawala kesi ya Kabendera

INATOKA UK. 2

itafanyika kesho (leo) saa 6:00 mchana na kwamba baada ya hapo familia itasarifisha mwili kwenda kuzika Bukoba, kwa kuwa uhusiano na mama na mtoto ni muhimu sana mahakama itoe kibali kwa mshtakiwa.

"Mheshimiwa hakimu, mshtakiwa kuhudhuria mazishi au maombi ya sala ya mwisho ya mama yake ni haki yake ya msingi ya kuheshimu familia chini ya Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977," alidai na kuongeza:

"Kwa kumzuia kushindwa kutoa heshima za mwisho au kumzika mama yake tutakuwa tunamwadhibu na adhabu hiyo ni kubwa sana katika maisha yake kwa sababu alipokuwa nje alikuwa akimlea na kumuuguza mama yake. Ni vyema akaruhusiwa kwenda kutoa heshima za mwisho," alidai Kambole wakati akiwasilisha maombi madogo mbele ya Hakimu Mtega.

Akifafanua maombi yake, alidai kuwa mama mzazi ni mmoja, amekufa mara moja kwa hiyo ni muhimu kwa mshtakiwa kuhudhuria tukio hili muhimu.

Hata hivyo, Wankyo alidai kuwa upande Jamhuri unasikitika na kuungana na Kabendera katika msiba huo mkubwa wa kuondokewa na mama yake mzazi na unatoa pole kwake na familia.

Kuhusu maombi madogo ya utetezi, alidai kuwa Jamhuri haina majibu kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza maombi kwa sababu mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi.

"Mheshimiwa Hakimu, mahakama yako tukufu inapaswa kujiuliza je, ni wakati sahihi? Na je, ina macho ya kisheria kutoa amri ya maombi ya utetezi?" Alihoji.

Simon alidai kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), hajatoa kibali kwa mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo mpaka upelelezi utakapokamilika, maombi hayo yamewasilishwa wakati si sahihi. Upande wa Jamhuri unaungana na utetezi katika masikitiko hayo katika msiba huo mkubwa.

"Mahabusi wengi wamekuwa wakipata misiba ya wapendwa wao, lakini hakuna utaratibu huo na kwamba mahakama ikufungua mlango huo itakuwa ni sababu kwa wengine maombi hayo yatupiliwe mbali," alidai Wankyo.

Mahakama hiyo ilikataa ombi la kwenda kutoa heshima au kuzika kwa kuwa haina mamlaka ya kusikiliza maombi hayo au mpaka ipokee kibali kutoka Mahakama Kuu.

Hakimu Mtega alisema mahakama yake imefungwa mikono na kwamba haina mamlaka ya kuingilia kesi yoyote ambayo iko kwenye hatua ya upelelezi kama inayomkabili Kabendera.

"Mahakama yangu inatupilia mbali maombi ya utetezi kwa sababu haina mamlaka ya kusikiliza maombi ya kesi ya uhujumu uchumi iliyopo kwenye hatua ya upelelezi," alisema.



Katika kesi ya msingi, ilidaiwa siku na mahali pasipofahamika mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari, 2015 na Julai, mwaka jana, mshtakiwa alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi.

Katika shtaka la pili, Kabendera anadaiwa kuwa anakabiliwa na shtaka la ukwepaji kodi wa Sh. 173,247,047.02.

Kabendera (pichani) anadaiwa kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 19, 2019, mshtakiwa huyo alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173,247,047.02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa kuwa kati ya Januari, 2015 na Julai, mwaka jana katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alitakatisha fedha kiasi cha Sh. 173,247,047.02.

**WAKILI ANENA**

Katika ukurasa wake wa Twiter, Wakili wa Kabendera aliandika: "Tumefanya jukumu letu na kesho (leo) saa sita mchana tutamuaga Mama Mujwahuzi Kanisa la RC Chang'ombe. Ni masikitiko yetu hatutakuwa na Erick, lakini tutaendelea kutimiza wajibu wetu kama mawakili."

**FAMILIA YAOMBA MSAADA**

Taarifa ya famili iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii ilieleza kuwa taratibu za mazishi zinafanyika nyumbani kwa mkwe wa marehemu na kwamba bajeti ya safari kutoka Dar es Salaam kwenda Bukoba na gharama za mazishi ni Sh. milioni 18 na familia imefanikiwa kukusanya Sh. 4,835,000.

"Kama Erick asingekuwa rumande tunaamini kwamba labda msiba huu usingetokea sasa na hata kama ungetokea, makali yasingekuwa hivi yalivyo," ilisema na kuongeza:

"Kama raia tunaoguswa na hali hii, tunaombwa tusaidie kupunguza makali haya kwa kutoa mchango wa pesa, kila mtu kadiri atakavyoweza ili kuwezesha mazishi ya mama wa Erick."


## Press Release

**Visiting Pakistan Navy Ship "PNS MOAWIN" to Host Free Medical Camp at Almuntazir Girls School, United Nations Road, Upanga, Dar es Salaam, from January 4-5, 2020**



The Pakistan Navy Ship PNS MOAWIN, as part of goodwill visit to the Port of Dar es Salaam, United Republic of Tanzania, from January 3-6, 2020, will be holding a 'Free Medical Camp' during her stay in Dar es Salaam.

The Medical Camp is being organized for two days at Almuntazir Girls School, United Nations Road, Upanga, Dar es Salaam, from 10 AM to 02 PM on January 4-5, 2020.

PNS MOAWIN is embarked with specialized Medical Team and free medicines sponsored by the Pakistan Navy. The Specialist doctors include Medical Specialist, Surgical Specialist, Anesthetist, Pediatrician, Pathologist and Dental Surgeon as well as laboratory test facilities.

The Medical Team of PNS MOAWIN is excited to welcome and extend the medical service to the friendly People of the United Republic of Tanzania.

**Pakistan High Commission, Dar es Salaam**

215572402


# Usafiri wakwamisha kesi ya vigogo IPTL

INATOKA UK. 3

Kadushi alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 2014, mahali tofauti jijini Dar es Salaam, Sethi, Makandege na Rugemarila walikula njama ya kutenda kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la kwanza washtakiwa wote watatu, waliratibu genge la uhalifu kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe binafsi.

Nchimbi alidai, Makandege anakabiliwa na shtaka la 13, kwamba kati ya Januari 23 na Februari 10, 2014, katika Benki ya Stanbic tawi la Centre lililoko Wilaya ya Kinondoni na Benki ya UBL (T) Ltd iliyoko Wilaya ya Ilala, mshtakiwa alijipatia kwa njia ya udanganyifu Dola za Marekani 380,000 na 600,000.

Katika shtaka la 14, Jamhuri ulidai kuwa katika Benki ya Stanbic na UBL, Makandege aliisabishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.

Wankyo alidai katika shtaka la 15, siku na tarehe ya tukio la 13, Makandege alitakatisha Dola za Marekani 980,000 wakati akijua ni zao la genge la uhalifu.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na uliomba tarehe nyingine ya kutajwa na kumuunganisha mshtakiwa na wenzake.

Katika kesi hiyo, Sethi na Rugemarila walifikishwa mahakamani hapo mapema 2017 wakikabiliwa na mashtaka 12 ikiwamo kula njama na kutakatisha Sh. bilioni 309 na Dola za Marekani 22,198,544.6 mali ya Serikali ya Tanzania.

Sethi na Rugemarila, wanadaiwa kutenda makosa hayo katika Jiji la Dar es Salaam, nchini Afrika Kusini, Kenya na India. Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao walikula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi, kutoa nyaraka za kughushi.

Pia wanadaiwa kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. bilioni 309.

# Wasafiri wa anga wapata unafuu

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

UBORESHAJI miundombinu ya usafirishaji ukiwamo wa sekta ya anga umeanza kupunguza gharama na usumbufu kwa wasafiri wanaotoka na kuingia nchini.

Miundombonu iliyoanza kuboreshwa na kuleta tija na unafuu huo ni pamoja na unaoendelea katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro ambao sasa umeanza kuvutia mashirika ya ndege ya nchi mbalimbali kuongeza safari za moja kwa moja kuja nchini, kupitia uwanja huo badala ya kupitia nchi jirani.

Hatua hiyo, licha ya kuchangia kuongeza watalii wanaokuja nchini ambao sasa wanatumia muda mfupi na gharama nafuu pia imetoa ahueni kwa Watanzania wanaosafiri kwenda nchi mbalimbali kwa ajili ya shughuli za kikazi, biashara na pia masuala ya kidini.

Wakizungumzia hali hiyo baadhi ya wananchi walioanza kunufaika wakiwamo wanaokwenda nchini Israel kila mwaka kwa ajili ya masuala ya kidini, wamesema hatua hiyo wameishukuru serikali ya awamu ya tano na kuiomba kuendelea kutekeleza miradi inayowapunguzia gharama za maisha na usafiri. Mmoja wa wasafiri hao akiwamo Mchungaji Dankan Ludovik, alisema kadiri muda unavyokwenda gharama za kwenda nchini Israel zinaendelea kupungua na pia muda wa safari pia umepungua kutokana na kuwapo kwa ndege za kutoka Kilimanjaro hadi nchini humo. Baadhi ya wadau wa sekta ya usafirishaji akiwamo Samson Keshama, kutoka kampuni ya utalii ya Excelent Guides, alisema kwa sasa muda wa usafiri wa kutoka Tanzania kwenda Israel umepungua kutoka saa tisa ya awali hadi kufikia saa manne na nusu. Kwa mujibu wa Samson kutokana na hatua hiyo ya serikali, kampuni ya Excelent Guide imetengeneza utaratibu wa kuwaunganisha Watanzania wanaokwenda Israel kwa ajili ya shughuli za kidini wakiwamo wanaotembelea maeneo muhimu ya ibada.

Alisema kupitia utaratibu huo pia gharama za usafiri zimeendelea kupungua na mwitikio wa wananchi unaendelea kuwa mkubwa mwaka hadi mwaka.

Naye Anold Lema ambaye ni kiongozi wa dini kutoka jijini Dar es Salaam, alisema kupungua kwa gharama hizo pia kumechangiwa na jitihada za serikali za kuzijengea uwezo taasisi zake na kuboresha utendaji wake wa kazi.

Alizitaja baadhi ya taasisi zilizoboreshwa na kuanza kuonyesha tija kubwa kuwa ni pamoja na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ambayo imeonyesha uwezo na mafanikio makubwa ya kutangaza utalii wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Wasafiri wengine waliozungumzia mafanikio hayo ni pamoja na Deus Kurwa na Danford Mwankiraa, ambao wameshauri nguvu zaidi kuongezwa kutumia ofisi za kibalozi kutangaza vivutio vya utalii hasa wa utamaduni.

Pamoja na hatua hiyo ya serikali ya kuboresha viwanja vya ndege ukiwamo wa Kilimanjaro kuanza kuwa na tija kwa mashirika makubwa ya kimataifa pia imeanza kuwanufaisha wananchi waliowekeza kwenye sekta ya utalii.

Baadhi ya wananchi hao pamoja na kuendelea kumpongeza Rais John Magufuli kwa hatua hiyo, wamesisitiza umhimu wa jitihada hizo pia kufanyika kwenye viwanja vingine vilivyoko kwenye maeneo yenye fursa za utalii hasa wa kiutamaduni.

# Mvua yabomoa daraja la mwaka mmoja

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MVUA kubwa zilizonyesha siku tatu mfululizo wilayani Masasi mkoani Mtwara, zimesababisha kubomoka kwa daraja la Mto Mkoo katika Kijiji cha Mkumbululu Kata ya Mchaulu, ambalo lilijengwa ndani ya mwaka jana.

Matengenezo ya daraja hilo yaliyofanywa na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), yaligharimu Sh. milioni 530.

Kubomoka kwa daraja hilo kumesababisha wananchi wa vijiji vya kata ya Mchaulu na kata za jirani ikiwamo Luatala na vijiji vya Wilaya ya Newala kushindwa kuvuka, huku magari yakibadilishana abiria na kurudi katika eneo hilo.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, akiwa na wajumbe wengine wa kamati ya ulinzi na usalama wa wilaya hiyo, alifika katika daraja hilo na kuzungumza na Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mtwara, Locadius Kambale, ili kufanya matengenezo ya haraka.

Mzee alisema Tanroads kwa kushirikiana na mkandarasi ambaye ni kampuni ya AGM Construction- LTD iliyojenga daraja hilo wameanza kufanya ukarabati wa muda wa kurejesha hali iliyokuwa awali.

Alisema serikali haipendi kuona ikitoa fedha nyingi kujenda madaraja halafu muda mfupi yanabomoka na kusababisha hasara kwa serikali na adha kwa wananchi.

"Naomba huu ukarabati ufanyike kwa haraka ili wananchi waweze kuvuka na kueleza kufanya shughuli zao kama kawaida," alisema Mzee.

Alisema athari zilizojitokeza kufuatia daraja hilo kukatika ni wananchi wa vijiji vya kata ya Mchaulu na Luatala pamoja na magari kushindwa kuvuka kupitia daraja hilo.

Mhandisi Kambale alisema daraja hilo lilijengwa kwa viwango vyote, lakini mvua kubwa iliyonyesha ilisababisha maji kujaa katika mto huo na kuharibu kingo za daraja.

Alisema mvua hiyo ilisababisha maji kufurika hadi kiwango cha juu na daraja mzima kujaa maji hadi iliyopelekea maji hayo kupita juu ya daraja na kuharibika kingo hizo kisha daraja.



Mchuuzi wa mboga aina ya kabeji ambaye jina lake halikupatikana akitafuta wateja kama alivyokutwa eneo la Uhindini jijini Dodoma jana. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# 'Jengeni utamaduni kuwajali wagonjwa'

**Na Elisante John,** SINGIDA

TAASISI za kidini nchini, zimetakiwa kujenga tabia ya kuwatembelea wagonjwa waliolazwa hospitalini ili pamoja na mambo mengine, kuwapa faraja na kuwapatia misaada ya kibinadamu.

Fursa hiyo pia itawawezesha kuwaeleza wagonjwa habari zenye matumaini ya maisha yao juu ya neno la Mungu.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Taasisi ya Dini ya Kiislamu ya Istiqama Tanzania, Tawi la Manyoni mkoani Singida, Sheikh Sultan Nassoro, alipokabidhi msaada wa kibinadamu kwa wagonjwa waliolazwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Manyoni.

Alisema kwa kufanya hivyo ni sawa na sehemu ya ibada pia ni ufahari na upendo kwa jamii inayokabiliwa na changamoto za maisha na maradhi, hivyo kwenda sawa na maagizo ya vitabu vitakatifu.

Sheikh Nassoro alibainisha kuwa msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli, katika kuwatumikia Watanzania kwa moyo mkuu kutokana na miradi mingi na mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa sehemu zote nchini.

Akipokea msaada huo kabla ya kuwapatia walengwa, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, aliishukuru taasisi hiyo na akatoa rai kwa wadau wengine kuendelea kushirikiana na serikali ili kutatua changamoto zinazowakabili baadhi ya Watanzania.

Mwagisa alibainisha kuwa ni vyema Watanzania, mashirika, wadau na taasisi mbalimbali zenye uwezo kuimarisha ushirikiano katika kusaidia sekta muhimu nchini, zikiwamo za afya, elimu na hata masuala ya mazingira ili kuchochea kasi ya maendeleo.

Baadhi ya wagonjwa waliolazwa katika hospitali ya wilaya hiyo, Daudi Mabala na Paulina Julius, waliishukuru Istqama kwa msaada huo kwamba utachangia kuimarisha afya zao huku wakitoa wito kwa wadau wengine wa maendeleo kuonyesha moyo kama huo.

Baada ya makabidhiano ya msaada huo, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Furaha Mwakafwila, alisema hospitali hiyo ina uwezo wa kulaza wagonjwa 150 kwa siku, huku idadi ya wale wa nje ikiwa ni watu 150 hadi 200, kwa siku.

Msaada huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. miliomi mbili, unajumuisha vitu mbalimbali kama vyakula (mikate), juisi, maji ya chupa na sabuni kwa ajili ya kufanyia usafi.

# Tari yaokoa mabilioni ununuzi mbegu

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) imeokoa Sh. bilioni 5.4 ambazo zilitakiwa kutumika kwa ajili ya kununua miche ya michikichi ya kisasa 900,000 aina ya tenela na kugawiwa bure ikiwa ni mpango wa kuendeleza zao hilo mkoani Kigoma.

Badala yake, kwa kutumia wataalamu wake kutoka Tari Kihinga ambao wanatafiti michikichi, imezalisha mbegu hizo nchini na kugawa bure kwa taasisi za serikali na wakulima katika wilaya zote za mkoa wa Kigoma ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Akizungumza wakati ugawaji wa mbegu 50,000 za michikichi kwa Gereza la Kwitanga ambalo linapanda ekari 60,000 za zao hilo, Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema fedha hizo zimeokolewa baada ya watafiti hao kutumia utaalamu wao kuzalisha mbegu milioni 1.2 ambazo zilipaswa kununuliwa kutoka nje ya nchi.

Dk. Mkamilo alisema kuwa mbegu hizo ambazo kwa sasa zinatumika katika uzalishaji wa mafuta katika nchi mbalimbali, zinazozalisha mafuta ya mawese, zinauzwa wastani wa Sh. 6,000 hadi Sh. 8,000 kwa taasisi binafsi zinazoagiza kutoka nje ya nchi na baadhi ya wakulima wakubwa katika mkoa wa Kigoma walikuwa wakinunua mbegu hizo.

Alisema kwa kutumia watafiti kutoka Tari Kihinga, wameunganisha mbegu ya michikichi aina ya Dura iliyopandwa kwa muda mrefu na wakulima, lakini inatoa mafuta kidogo na Pesifela yenye ganda kubwa na kufanyiwa utaalamu kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mapipa na kuzalishwa mbegu ya tenela ambayo ndiyo inatumika katika nchi mbalimbali, ikiwamo Malyasia inayoongoza duniani kwa kuzalisha mafuta ya zao hilo.

"Licha ya kuokoa fedha za serikali mpaka sasa Sh. bilioni 5.4 ambazo zingetumika kuagiza mbegu za michikichi ya tenela, tunajivunia mbegu hizo zinazalishwa katika mazingira ya hapa hapa nchini ambazo zinamudu mazingira yetu," alisema.

Ofisa Kilimo katika Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma, Joseph Rubuye, alisema mkakati uliopo hivi sasa ni halmashauri zote kwa kushirikiana na Tari wameanzisha vitalu vya mbegu bora za michikichi ya tenela na kugawa bure kwa wakulima ili kuzalisha mafuta.

"Nasisitiza kila mkulima wa michikichi katika mkoa wa Kigoma atapewa miche bure katika halmashauri aliyopo. Cha muhimu ni kwenda kujiandikisha jina na kueleza anataka kupanda eneo la ukubwa gani. Sambamba na hilo, atapewa utaalamu na maofisa ugani wetu ambao tayari tumeshawapa mafunzo ya kutosha," alisema.

Mmoja wa wakulima, Pili Ryiyagazi kutoka Wilaya ya Kigoma, aliomba serikali kuharakisha usambazaji wa mbegu za kisasa za michikichi ya muda mfupi aina ya tenela ili kuongeza uzalishaji wa mafuta.

Alisema mbegu za zamani aina ya dura zilizokuwa zikitumika enzi za mababu zao, kwa sasa zimepitwa na wakati kutokana na kuchukua wastani wa miaka 10 kuanza uzalishaji na kwamba hata hao waliopanda miaka ya nyuma hawakunufaika.



Waziri wa Madini, Doto Biteko, jana, akishirikiana na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bunango, Kata ya Bugalama, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Kanjanja Kanjanja, kubeba mchanga wa madini uliotakiwa kuchenjuliwa kwa njia ya kiwanda bubu kilichopo katika kata hiyo. **PICHA NA SHABAN**

# Wanaswa tuhuma za uhalifu Mwaka Mpya

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga limewakamata watu mbalimbali kwa tuhuma za kufanya uhalifu katika sikukuu ya Mwaka Mpya.

Watu hao baada ya uchunguzi kukamilika watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii kuhusiana na operesheni hiyo ya kusaka wahalifu katika sikukuu ya Mwaka Mpya.

Alisema watu hao walikamatwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Tanga katika mkesha wa Mwaka Mpya na siku yenyewe ya Mwaka Mpya katika msako mkali wa Jeshi la Polisi.

Bukombe alisema watu hao walikamatwa kwa tuhuma za uzembe na uzururaji pamoja na makosa mengine mbalimbali ambayo wamefanya katika sikukuu ya Mwaka Mpya mkoani Tanga.

Katika mkesha huo na sikukuu yenyewe, alisema kulikuwa na ulinzi mkali katika makanisa yote ili kuhakikisha mambo yanakwenda sawa hususan suala zima la amani na utulivu.

Kamanda Bukombe alisema hali ilikuwa nzuri na hakuna matukio makubwa ambayo yametokea katika mkoa wa Tanga ya kufanya watu washtuke.

# Askofu ataka amani mwaka wa uchaguzi

**Na Jumbe Ismailly,** MANYONI

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Singida, Edward Mapunda, amezindua kituo kipya cha Hija katika Kijiji cha Sukamahela, wilayani Manyoni pamoja na kuadhimisha Siku ya Amani Duniani.

Akizungumza na waumini wa madhehebu ya Kikatoliki kwenye uzinduzi wa kituo hicho kilichoko Parokia ya Chibumagwra, Askofu Mapunda alisisitiza kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu.

"Mwaka huu taifa letu litakuwa na uchaguzi Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Wabunge na Madiwani kwa hiyo nawaalika tuiweke nchi yetu katika sala," alisema.

Aidha, askofu aliweka wazi kwamba kutokana na uchaguzi huo, ni wakati mwafaka sasa kuiweka nchi katika sala na kikubwa zaidi ni kuikabidhi nchi kwa Bikira Maria Mama wa Mungu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo kwa kufanya hivyo, uchaguzi huo utakuwa kwenye mikono salama na utakwenda vizuri kwa sababu yeye ni malikia wa amani.

"Tumwombee Rais wetu ambaye ametuchangia ujenzi wetu... alileta mchango wake kupitia Mkuu wa Mkoa wetu wakati anakwenda Chato kwenye mapumziko. Kwa hiyo tunamshukuru sana Rais Dk. John Magufuli kwa sala na michango yake mbalimbali," alisisitiza.

Askofu Mapunda aliweka bayana kwamba kituo cha hija kilichozinduliwa katika Kijiji cha Sukamahela ni cha pili baada ya kile cha Kijiji cha Kimbwi kinachotumiwa na waumini wa madhehebu ya dini ya Kikristo kwenda kuhija kwa kipindi cha kila mwaka.

Alisema baada ya kituo hicho kuzinduliwa, kutakuwa kukifanyika sherehe za kuiombea nchi amani na kumshukuru Mungu kila Desemba 9 ya kila mwaka.

Makamu Askofu wa Jimbo la Singida, Padri Francis Limu, awali alibainisha kuwa pamoja na wengine wote aliomba kuwataja wawili ambao ndio walikuwa waanzilishi wa wazo hilo ambao ni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi na Askofu Mapunda.

"Waliwaza hapa Sukamahela iliyo katikati ya Tanzania kiwapo kitu fulani cha kiroho, ndiyo wazo la kwanza. Pia kiwapo kitu fulani cha kiroho ambacho kinaonyesha upekee mahali hapa kijiografia," alisema.

# Wajasiriamali watakiwa kuboresha vifungashio

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo na kati nchini, wameshauriwa kuboresha vifungashio vya bidhaa wanazozalisha, ili kuvutia soko la ndani na nje ya nchi.

Wito huo umetolewa jana na Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Arusha, Nina Nchimbi, wakati wa kufunga mafunzo ya wiki moja kwa wajasiriamali wa kutengeneza sabuni za maji na kipande, dawa za kuua wadudu chooni na dawa za kusafisha vigae. Nchimbi alisema wajasiriamali wanapaswa kuwa wabunifu kila wanapozalisha bidhaa zao, ili kuongeza ubora katika biashara zao na kuwavutia wateja zaidi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema wengi wanajitahidi kuzalisha, lakini changamoto kubwa ni uboreshaji wa vifungashio ambao aliwataka kumalizwa na wabunifu zaidi. "Unapozalisha bidhaa yako kila wakati inakuwa na mwonekano ule ule, inakuwa ngumu kupata wateja wapya na ili kupata wateja wapya, ni lazima mbadili mwonekano wa vifungashio viwe vya tofauti na zivutie wateja na kwa kufanya hivyo, mtapata soko la uhakika," alisema Nchimbi.

Naye Mkufunzi wa Mafunzo hayo, Bahati Mkopi, alisema ujuzi unaotolewa ni wa kutengeneza sabuni na kwamba ni awamu ya nne sasa na zaidi ya wajasiriamali 80, wamehitimu mafunzo hayo na kuleta manufaa makubwa, ikiwamo kuanzisha viwanda vidogo na vya kati zaidi ya 10.

Alisema mafunzo hayo yamewasaidia vijana kujiajiri na kupata uhakika wa kipato kwa kujishughulisha wenyewe.

Mmoja wa wajasiriamali akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mboka Mwakalinga, alisema kupitia mafunzo hayo wamepata utambuzi wa kitaaluma ya vyeti ambavyo vitawawezesha katika mambo ya usajili, na kuanzisha viwanda vidogo.




Mnunuzi akiwa anachagua bidhaa za vifaa vya umeme kwa ajili ya kununua. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Sita wazaliwa mkesha Mwaka Mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WATOTO sita wamezaliwa kwenye Kituo cha Afya Mirerani wilayani Simanjiro na Hospitali ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, katika mkesha wa Mwaka Mpya wa 2020.

Mganga Mfawidhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Dk. Malkiad Mbota, aliiambia Nipashe kuwa kati ya watoto hao wawili walizaliwa kwenye hospitali ya wilaya hiyo na kwamba mmoja wa kike na kiume.

Naye Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mirerani, Dk. Hassan Ishabailu, alisema watoto wanne walizaliwa kwenye kituo hicho. Alisema kati ya watoto hao wanne, wawili ni wa kike na wengine wa kiume na kwamba wote na wazazi wao wanaendelea vizuri.

Mmoja kati ya wazazi waliojifungua, Mariam Hussein, alisema anafurahia kwa kuanza vyema mwaka mpya kwa kupata mtoto wa kiume.

"Hivi sasa kuna huduma nzuri kwenye Kituo cha Afya Mirerani, jengo la mama na mtoto na vifaa vya upasuaji na wauguzi na madaktari wanatusaidia bila tatizo," alisema.

# DC Muro kutatua migogoro ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya Arumeru, Jerry Muro, amewahakikishia wananchi wake kuwa ataendelea kutatua changamoto zinazowakabili kwa haraka ikiwamo changamoto za ardhi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wilayani humo, kuhusiana na migogoro inayowakabili ya ardhi na kusababisha mtafaruku kati ya ndugu na jamaa na hata kukosekana kwa amani kwenye jamii yao.

Alisema ofisi yake imeweka mkakati wa kutatua kero za wananchi wake na ofisi yake imeweka wanasheria wanne, ambao watawasaidia wananchi wasiokuwa na uwezo katika kesi zao mahakamani.

"Kuna baadhi ya wananchi ambao wana kesi mbalimbali na wanataka msaada wa kisheria, lakini wanashindwa kuweka wanasheria kutokana na kutokuwa na uwezo, hivyo nimeamua kuwatafutia wanasheria hawa wanne, ambao nitawalipa kwa mshahara wangu, ili wafanye kazi yakutatua matatizo ya wananchi yanayohusu sheria," alisema Muro.

Akizungumza na wananchi Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana aliyeambatana na Muro, aliwahakikishia wananchi wa Meru kuwa atamwondoa askari yeyote atakayekiuka taratibu na kanuni za kazi yao kwa kuchafua sifa za Jeshi la Polisi kwa kujiingiza katika migogoro ya ardhi.

"Napenda kuwaahidi wananchi kuwa sitamfumbia macho askari yeyote, atakayekiuka sheria na mwananchi atakayeona askari yoyote anakiuka sheria, chukua simu nipigie nimshughulikie, naahidi nitasimamia vyema hili," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Emmanuel Mkongo, alimhakikishia kamanda huyo kumpa ushirikiano katika kazi zake za ulinzi na usalama.



## UVCCM Siha wapata bosi mpya

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KADA wa Chama Cha Mapinduzi, Yohana Lengere, maarufu 'Laitayo', ameukwaa Uenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) Wilaya ya Siha, baada ya kumwangusha mpinzani wake wa karibu kwa tofauti ya kura 30.

Lengere alitangazwa mshindi katika uchaguzi huo uliofanyika wilayani hapa jana, baada ya kupata kura 86, akifuatwa na mpinzani wake John Mushi, aliyepata kura 56, huku mgombea mwingine Gema Mtui akiambulia kura moja.

Akitangaza matokeo hayo, Katibu wa UVCCM Wilaya ya Siha, Bulugu Magege, alisema uchaguzi huo ulikuwa huru na wa haki na hakuna mgombea aliyelalamika kuchezewa rafu.

"Tunamshukuru Mungu kwamba tayari tumempata mwenyekiti wa jumuiya yetu na sasa tunajipanga kufanya kazi za chama kuelekea uchaguzi mkuu ujao wa Rais, wabunge na madiwani utakaofanyika baadaye mwaka huu.

"Kimsingi, uchaguzi wetu ulikuwa huru na wa haki na mpaka sasa hakuna aliyelalamika kuchezewa rafu wala kukata rufani kupinga mchakato mzima uliyofanyika. Yohana Lengere kwa sasa ndiye Mwenyekiti wa UVCCM wa Wilaya ya Siha," alisema.

Lengere anarithi mikoba ya Wilson Mushi, aliyelazimika kujiuzulu katika nafasi hiyo baada ya kuajiriwa serikalini kuwa Ofisa Mtendaji wa Kata (WEO).

Kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo, Magege alionya kuwa uchaguzi huo unapaswa kuwa mchezo wa kirafiki, kwa kuwa wote ni wana CCM na hakuna sababu ya kuwapo na hila, fitina, wala kuvunjana miguu kwa wagombea na wafuasi wao wanaowaunga mkono.

Uchaguzi huo ulikuwa ukivuta hisia za wananchi wa Siha hasa kutokana na wagombea wa nafasi hiyo kuonyesha hamasa kubwa wakati wa kuchukua na kurudisha fomu.



Madereva wa bodaboda wakionekana kuendesha vyombo hivyo bila kuwa na kofia ngumu pamoja na wateja wao, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao na abiria hao wanaotumia usafiri huo, kama walivyokutwa jana, jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakubaliana Kilimanjaro iwe Dubai ya Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZAWA wa Moshi takribani 900, wakiwamo wafanyabiashara maarufu wanaoishi ndani na nje ya nchi, wamepitisha maazimio 17 watakayoyapigia chapuo mwaka huu ili kuifanya Kilimanjaro kuwa Dubai ya Tanzania.

Maazimio hayo yalipitishwa na wazawa hao wakati wa kikao cha waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini kilichoongozwa na Mkuu wa Kanisa hilo nchini, Askofu Dk. Fedrick Shoo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, Arthur Shoo, maazimio hayo yalifikiwa Desemba 27, mwaka jana, wakati wa kikao cha Askofu Dk. Shoo na wana Dayosisi ya Kaskazini.

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa mnenaji mkuu wa kikao hicho alikuwa ni Askofu Shoo ambaye katika hotuba yake aligusia mambo muhimu ya dayosisi hiyo na mipango yao ya mbeleni.

"Ni kweli tulikuwa na huo mkutano na moja ya mambo yaliyoazimiwa na wana dayosisi waliopo nje ya Kilimanjaro ni kwamba KKKT ifungue kampuni ya kitalii inayoweza kuwekeza pia kwenye hoteli za kisasa na kuitangaza duniani.

"Na tumekubaliana tuanze na fursa zilizopo, mfano kwa kuanzisha kilimo chenye soko duniani, kilimo cha parachichi, yaani green gold," alisema.

Katika taarifa yake hiyo, Katibu Mkuu huyo pia alisema wazawa hao wameazimia kuanzisha kituo cha uwekezaji ili kusaidia kanisa kutengeneza wajarisiriamali na wawekezaji na kuwa na njia za moja kwa moja za kuwafikia wale wenye uchumi duni.

Alisema waliazimia kuifanya Kilimanjaro kuwa Dubai ya Tanzania, kuunda sekretariati ya kuratibu mawazo katika mikutano hiyo na kutoa mrejesho, lakini Benki ya Uchumi (UCB) inayomilikiwa na KKKT Dayosisi ya Kaskazini, ifanye kazi kibiashara ili kufikia wakristo katika usharika na taasisi zake sita.

Aliongeza kuwa wamekubaliana kukitangaza Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stefano Moshi (SMMUCo) kwa nguvu zaidi na kanisa kuwekeza katika rasilimali watu watakaoendesha vyuo vyao.

Alisema wazawa hao wa Moshi wameeleza kuwa ajira hazipo ila kazi zipo nyingi, hivyo wanataka kuanza kuwafundisha watoto kazi za nyumbani ili kuwajengea misingi ya kujiajiri.

Azimio lingine ni kanisa liongeze bidii katika kutumia wataalamu wake katika kuimarisha uchumi na elimu kwa jamii na kuwapo ufadhili kwa watoto katika shule za awali.

Alisema wameazimia kanisa hilo liongeze ubora wa elimu kwa kuongeza masomo ya lugha mbalimbali zinazofundishwa kama Kijerumani, Kifaransa na kuanzisha mafunzo ya vitendo.

"Kwa ujumla, tunataka kuwa na mtaala unaojengea wanafunzi uwezo wa kimaisha na pia vyuo vyetu vikuu viwe na kampuni za kibiashara na uwekezaji na pia elimu ya sekondari iwe bora ili kupata wanafunzi wenye sifa na uwezo mzuri.

"Tuwe na 'active website' (tovuti inayofanya kazi) ya dayosisi kwa ajili ya kushirikishana haya mambo mazuri, masomo ya dini yaingizwe kwenye mtaala wa shule na wanafunzi wake watahiniwe.

Lakini pia kanisa litumie nguvu yake ili somo la dini liingizwe shuleni kwa kushirikiana na serikali," sehemu ya taarifa hiyo ilisomeka.

# Kaya 34 zagomea amri halmashauri Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

KAYA 34 zinazomiliki mashamba ya kilimo katika eneo la Ngurunga, Kata ya Hedaru wilayani Same mkoani Kilimanjaro, zimegoma kuhama na kuondoa mazao katika eneo hilo, baada ya kuamriwa na halmashauri ya wilaya hiyo kusitisha shughuli zote za kilimo kuanzia sasa.

Kutokana na kutolewa kwa amri wanayodai ina utata, wakulima hao wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati, wakidai walishapewa haki mara mbili na mahakama.

Mkazi wa Kijiji cha Gundusine anayemiliki shamba katika eneo Ngurunga, Yohana Hondo, alisema wanashangazwa na hatua ya Halmashauri ya Wilaya ya Same kuwaandikia barua ya kuwataka kuacha kulima ndani ya mashamba yao kwa madai kuwa ni eneo la Msitu wa Hifadhi wa Lungwana Ngurunga.

"Hatuelewi kwanini wanatuamuru kuacha kulima na kufanya shughuli za kilimo katika maeneo yetu ya asili ambayo tuliachiwa na wazee wetu na wakati kuna chakula shambani.

"Tuliwashinda kesi mara mbili mahakamani, moja ikiwa ni Baraza la Ardhi la Kata ya Hedaru na nyingine ni Mahakama ya Ardhi ya Wilaya. "Tunaonewa, tunanyanyaswa na wanataka kudhulumu haki yetu. Hii si sawa hata kidogo, tunamwomba Rais John Magufuli atusaidie kupata haki yetu kwa sababu anasaidia wengi," alisema.

Katika barua ya Halmashauri ya Wilaya ya Same yenye kumbukumbu namba SDC/F.40VOL.XIV/22 ya Desemba 16, 2019, inaelekeza kusitishwa kwa shughuli za kilimo katika eneo hilo.

Amri hiyo ya serikali imefafanua kuwa kufanya shughuli za kilimo katika eneo hilo ni kukiuka sheria ndogo zilizopitishwa na vikao vyote halali vya kijiji, kata na wilaya pamoja na Sheria ya Misitu ya Namba 14 ya Mwaka 2002.

Pamoja na mambo mengine, katika barua hiyo, imetahadharishwa kuwa endapo wananchi hao watakaidi amri hiyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Simon Samweli na wenzake.

Kwa mujibu wa barua hiyo, eneo la Lungwana Ngurunga ni eneo la msitu wa hifadhi na mchakato wa kuuhifadhi ulianza rasmi mwaka 2011 na kukamilika mwaka 2017 na sheria ndogo ilitiwa saini Machi 31, 2017. Jana,

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alipotafutwa kuzungumzia mgogoro huo kati ya wananchi na halmashauri, aliahidi kuwa atatoa ufafanuzi leo mchana.



Simulizi aliyepona kwa dawa asili, sasa muuzaji wake maarufu

Ukurasa 18

# BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ijumaa Januari 3, 2020
Nipashe



## HATIMAYE INAFUFULIWA...
## Neema msaada wa Japan kurejesha Tafico, mapya soko la samaki kitaifa

Ukurasa 14



WAPOKEA SALAMU ZA JPM

# TARI YAJA NA MPANGO MKAKATI WA MBEGU BORA MAZAO KUFIKA TANZANIA YA VIWANDA

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

HATIMAYE INAFUFULIWA...

# Neema msaada wa Jap Tafico, mapya soko la

• Zama zaja samaki kufuatwa bahari kuu



Meli iliyokamatwa katika Pwani ya Mtwara ikiwa na samaki iliyowapata kinyume cha Sheria ya Usimamizi wa Bahari Kuu(DSFA) ya Mwaka 1998. Ilitozwa faini ya Sh. milioni 770. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

SERIKALI ya Japan imetoa msaada wa Yen (sarafu ya Japan) milioni 200 (sawa na Sh. 4.2 bilioni za Tanzania) kusaidia kufufuliwa kwa Shirika la Taifa la Uvuvi (Tafico) lililozimika mwaka 1998.

Ni habari njema ya Tafico kurejea mahali pake, baada ya kuwa na jina kubwa katika kipindi cha zama zake.

Kaimu Balozi wa Japan nchini, Katsutoshi Takeda, alitia saini makubaliano hayo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Doto James, hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kama sehemu ya misaada ya Japan kwa maendeleo ya taifa hili.

Katibu Mkuu alisema katika hafla hiyo kuwa, msaada huo utatoa mchango katika kufikia Malengo ya 2025 na Mkakati wa Maendeleo Endelevu 2030, pia Ajenda ya Maendeleo Afrika, 2063.

Chini ya mradi huo, mambo mengi yatafanywa ikiwa ni pamoja na kufukua meli ya uvuvi yenye uwezo wa kuweka katika barafu shehena ya siku tano ya samaki.

Itakuwa na mtambo ya kutengeneza barafu, chumba baridi cha uhifadhi, zana za uvuvi, karakana ya mahitaji baharini, gari la kusafirisha mizigo barafu na la kawaida la kuwasilisha samaki.

Meli hiyo inawekewa matumaini kusaidia kufufua mchango wa sekta hiyo katika uchumi, ingawa inawezekana haina uhusiano wa moja kwa moja na mahitaji mengine ya sekta hiyo, maana haikufafanuliwa.

Moja ya matokeo yanayotazamiwa kutokana na mradi huo, ni kuongeza uuzaji nje wa samaki na kuongeza kiwango cha usalama wa chakula nchini, pamoja na kuongeza kiwango cha kusindika samaki.

Aidha, kuna kuongeza thamani na kupunguza upotevu baada ya kuvua. Bado hata hivyo changamoto zipo, kwa mfano za kufanya doria maeneo ya bahari-ni, eneo la ukanda wa kiuchumi kwa upande wa Tanzania, meli za kigeni zisivue ovyo.

Maeneo mengine ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalenga kuhusu sekta ya uvuvi kuhusiana na mradi wa kuifufua Tafico, ikiwamo umuhimu wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi.

Kuna mkakati vilevile wa kuongeza jitihada za kushirikisha jamii za wavuvi katika kudhibiti matumizi ya rasilimali samaki kwa ushiriki wa makundi wakati serikali ikiboresha miundombinu ya uvuvi.

Hapo kuna maeneo salama pa kufikiwa na mitumbwi, wavuvi wakitoka baharini au katika ziwa na shehena ni mojawapo ya miradi hiyo.

Kukua kwa sekta ya uvuvi kunaakisiwa kufikia asilimia 9.4 mwaka 2018 ambayo iliongezeka kiasi kutoka asilimia 8.4 mwaka 2017 na wataalamu wizarani wanasema hali hiyo ilitokana na usimamizi bora zaidi wa maeneo ya mazalia ya samaki.

Ni pamoja na kampeni za 'hapa kazi tu' za kuondoa vianzio kadhaa vya uvuvi haramu, kuanzia nyavu nyembamba hadi utumiaji baruti.

Halafu kuna suala la kuongezeka mikopo ya benki na kukubalika kwa dhamana, kunawawezesha watu binafsi kuanzisha mabwawa ya kuzalisha samaki, hatua endelevu kuliko kufufua shirika kubwa.

Suala la Tafico kuongeza upatikanaji wa samaki katika soko la ndani na uuzaji nje, ndiyo hasa linalopaswa kuangaliwa katika mapana yake ya kiuchumi, kutarajia.

Pia, kama msaada wa Japan utaleta tija kubwa zaidi katika uchumi kwa kufufua shirika. Uvuvi bado unachangia kiasi cha asilimia 1.7 katika uchumi wa taifa kwa takwimu za 2018, licha ya bahari, maziwa, mito.

Zikiangaliwa takwimu husika, sasa inakaribia kutimu miongo sita baada ya uhuru wa nchi kuwapo kwa vyanzo vyote vya shughuli za uvuvi kitaifa, lakini bado sekta hiyo inaelezwa kuchangia asilimia1.7.

Hapo inazaa picha sekta ya uvuvi tija yake haijafikia kilele kama ilivyo katika kilio cha kilimo, kuwa suala ni mazingira ya kazi, nyenzo na kiasi cha uhitaji wa samaki katika soko na bei ambazo walaji wanamudu kununua zina mchango wake.

> **Moja ya matokeo yanayotazamiwa kutokana na mradi huo, ni kuongeza uuzaji nje wa samaki na kuongeza kiwango cha usalama wa chakula nchini, pamoja na kuongeza kiwango cha kusindika samaki.**

Kutatua suala la uwezo wa kununua samaki, ni suala linalohitaji angalizo la soko katika namna yake. Kimsimgi, kuongezeka upatikanaji samaki katika soko la ndani, haitoshi tu kupitia uvuaji kwa wingi, ila pia wauzwe kwa bei ndogo na shirika lipate faida.

**UHAI WAKE**

Kwa kufanya hivyo, kunaifanya taasisi hiyo ya uvuvi kurudisha gharama zake na kujiendesha kwa tija na faida.

Ni kawaida gharama za uendeshaji za mashirika ni kubwa na inapokuwa kubwa bila ya tija, iko wazi haitoweza kumudu uuzaji wa bidhaa zake kwa bei ndogo, ili kumudu kupanua idadi kubwa ya wateja iliyo nayo.

Iko wazi Tafico ikianza kazi

# pan kurejesha samaki kitaifa



itadai kulindwa kisoko, kuzuia samaki kutoka nje wasiuzwe hasa katika masoko ya ndani, lengo ni kuiweka imudu ushindani na kujiboresha kibiashara, kwa manufaa ya Watanzania.

Mtu anaweza kwenda mbali zaidi na kuangalia mustakabali wa kiuchumi na misaada ya Japan kwa upande huo na tija yake.

Katibu Mkuu Dotto anasema, tangu mwaka 2012 Japan imeipatia Tanzania misaada na mikopo nafuu inayofikia Sh. trilioni1.3, kuwezesha miradi ya sekta za kilimo, barabara, maji, nishati, utawala bora na uwajibikaji.


Pia kuna miradi mingine iko njiani iliyopangiwa Yen 37.9 bilioni au sawa na Sh. 784.57 bilioni, ambayo bado haijatiwa saini. Mtazamo wa kimaendeleo unakua. Ni kwa kiasi gani itasaidia kuondoa umaskini.

Ni wazi, wataalamu na washauri wa kifedha, kuchumi na maeneo yanayofanana kwa jumla, wanafanya kazi zao. Huku wakiiona Tafico ni shirika muhimu kwa haiba ya uchumi wa nchi na wizara husika.

Changamoto ninayoiona mbele ni kwa kiasi gani, Tafico mpya itafika katika ng'ambo ya kufanikisha uvuvi wenye tija ya bei, ubora na upatikanaji wa bidhaa kwa wateja wake.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James (kulia) na Kaimu Balozi wa Japan nchini Tanzania, Katsutoshi Takeda, wakibadilishana mkataba wa msaada kwa ajili ya kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), hafla hiyo iliyofanyika katika Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.



Hili ndilo zao la chia shambani na baada ya kuvunwa. **PICHA: MTANDAO.**

# Unalijua zao la chia? Pata darasa lake

**Na Sabato Kasika**

MOROGORO ni miongoni mwa mikoa inayotajwa kuwa na fursa nyingi za kiuchumi nchini, hasa zinazotokana na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara na chakula.

Baadhi ya mazao ya biashara na chakula yanayolimwa kwa wingi mkoani humo ni mpunga, mahindi, ufuta, maharage, viazi vitamu, alizeti, pamba, korosho, ndizi, miwa, mbaazi, choroko na matunda ya aina mbalimbali.

Kwa miaka mingi, wakazi wa mkoa huo wamejikita zaidi, katika kilimo cha mazao hayo, lakini sasa limeibuliwa zao lingine linalotajwa kwa jina la chia ambalo inaelezwa kuwa linaweza kuwaongezea kipato zaidi.

Zao hilo linatajwa kwa jina la chia, ambalo limeanza kulimwa kwenye baadhi ya maeneo ya mkoa huo, kwa vile hali ya hewa ya Morogoro inaruhusu kilimo cha chia kistawi kwa wingi.

Yawezekana chia likawa ni zao geni masikioni mwa wengi, kwa vile halijazoeleka, lakini linatajwa kuwa linatokana na aina ya mmea unaokaribia kufanana na ufuta, huku likiwa na mbegu kama mchicha.

Inaelezwa kuwa chia imekuwa ikitumika kama chakula na dawa ya magonjwa mbalimbali kwa makabila ya Aztecs na Mayans kutoka Amerika ya Kusini, ambako ndiko kwenye chimbuko lake.

Mtu anaweza kuchanganya vijiko vya mbegu za chia katika uji, juisi au chakula chochote na baada ya dakika 10 hadi 30, anaweza kula chakula hicho, ambacho huwa na mwonekano wa kuvutia kama mlenda.

Bismass Shilla, ni mkazi wa mkoa wa Morogoro anayesema ameamua kulima zao hilo, baada ya kubaini chia inaweza kulimwa mara tatu kwa mwaka na mazao yake ni bei kubwa.

Anasema, katika ekari moja ya chia, mkulima anaweza kuvuna magunia mawili hadi tatu, huku kilo moja ikifikia kuuzwa kati ya Sh. 10,000 hadi 15,000, hali ambayo ni rahisi kumwinua mkulima kiuchumi.

Shilla ambaye anatoka katika kituo cha Morogoro Chia Center, kilichoanzishwa Julai mwaka jana na kuwekeza katika kilimo cha chia, anasema kina wanachama 70 na zaidi ya ekari 140 za zao hili zimelimwa.

Mkulima huyo anasema, lengo la kuanzisha kituo hicho ni kukuza kilimo cha chia, kuuza na kununua ili kuongeza zao lingine la biashara mkoani Morogoro na kuinua kipato cha wakulima.

"Kilimo chake huchukua siku 90 tangu kupandwa hadi kuvunwa kama zao hilo litakuwa, lakini likikosa jua la kutosha, halikauki kirahisi na linaongezeka matawi na kuchukua miezi minne badala ya siku 90," anasema Shilla.

Anasema, udongo unaohitajika kwenye kilimo cha zao hilo ni udongo tifutifu na siyo wa mfinyanzi, kwa vile udongo mfinyanzi, unasababisha jua likiwaka, mizizi inashindwa kupenya vizuri katika ardhi.

Mkulima huyo anataja ardhi inayohitajika ni iliyochoka na barafu haiwezi kuota, lakini kwa maeneo kama Morogoro, Handeni, Moshi, Tukuyu na Kigoma, instawi kwa wingi.

Kwa mujibu wa taarifa za tovuti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Morogoro ina eneo la hekta 2,226,396 linalofaa kwa kilimo na kati ya eneo hilo, zaidi ya hekta 862,092 ndizo zinazolimwa kwa sasa sawa ambazo ni sawa na asilimia 39.

Vilevile eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji mkoani humo, linatajwa kuwa ni hekta 1,510,339.51, lakini eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni hekta 40,558, ambalo ni sawa na asilimia tatu.

Mkoa pia una mito 143 inayotitirisha maji mwaka mzima, udongo mzuri na mabonde mengi, ambayo bado hayajaendelezwa, hivyo ni fursa kwa wakazi wake kuangalia uwezekano wa kuinuka kiuchumi kupitia kilimo cha chia.

UCHUMI

WAPOKEA SALAMU ZA JPM

# Tari yaja na mpango mkakati wa mbegu bora mazao kufika Tanzania ya Viwanda

- Mkurugenzi: Matawi yote 17 yapewa cha kufanya 2020
- Naibu Waziri Mgumba: Tumewapa majukumu, kazi kwao

**Na Ashton Balaigwa, DODOMA**

UNAPOZUNGUMZIA safari ya Tanzania kuelekea uchumi wa kati, daima ni vigumu kuiruka sekta ya kilimo, ambayo daima haijawahi kuachwa katika mpango mkakati wa nchi tangu uhuru.

Nafasi ya kilimo iko katika sura kuu mbili, kuwahakikishia Watanzania mlo wa kila siku, pia malighafi ya mazao ya kilimo kwa viwanda.

Hivi karibuni Rais Dk. John Magufuli, alihimiza tena kilimo kiwe na mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi, kwa kuhakikisha kunazalishwa mbegu za mazao kimkakati hapa, ili kuwasaidia wakulima na kuiondoa nchi katika hali tegemezi ya mbegu kutoka nje.

Inaelezwa, kwa sasa asilimia 70 za mbegu zinatoka nje ya nchi na asilimia 30 iliyobaki ndio inazalishwa nchini, kiwango ambacho Rais Magufuli hakubaliani nacho, akilalamika hakiwezi kumletea tija mkulima.

Ameiagiza Wizara ya Kilimo, kupitia taasisi zake kuanza kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa, zitakazomnufaisha mkulima aongeze tija.

**TARI YANENA**

Kutokana na agizo hilo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), anasema wapo tayari kuzalishaji mbegu za teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kuondoa utegemezi, inayomwezesha mkulima kwenye kilimo cha kisasa, wakitumia mbegu bora na zenye gharama nafuu zaidi.

Ni kauli ya Dk. Mkamilo, baada ya kumalizika kikao kazi cha tathmini ya malengo na mikakati mipya, Tari iliyojiwekea, iliyohusisha wakurugenzi na mameneja wa vituo vya utafiti 17.

Anasema kwa kutumia mashamba ya taasisi hiyo, wanaweza kuzalisha mbegu bora za kuwasaidia wakulima zinazokabili magonjwa na kutimiza agizo la Rais Magufuli.

Dk. Mkamilo anasema, tayari baadhi ya vituo vya Tari vimepewa majukumu ya kuzalisha mbegu, kulingana na mazao ya maeneo yao na vimeshaanza uzalishaji wa kuwasaidia wakulima kupata mbegu hizo za teknolojia ya kisasa na sifa za kupambana na wadudu.

"Utafiti na kila kituo kimepewa mazao ya kimkakati, mfano kituo cha Naliendele- Mtwara kimepewa jukumu la kuzalisha mbegu za korosho, karanga, njugumawe na ufuta kwa ajili ya kuhudumia mikoa yote ya Kusini.

"Kituo cha Ilonga - (Kilosa) Morogoro kimepewa jukumu la kuzalisha mbegu za alizeti, mtama, mahindi, mazao ya mikunde na mazao ya mizizi kama viazi vitamu kwa mikoa ya kanda ya kati," anasema bosi huyo wa Tari.

Dk. Mkamilo, anasema umefika wakati wa kilimo kubadilika kutoka kwenye kujikimu kimaisha hadi lengo la kibiashara, ikichochewa na matumzi ya mbegu za teknolojia ya kisasa, pamoja na matumizi ya pembejeo kwa wakulima, hivyo kusaidia uzalishaji malighafi kitaifa.



Miche ya korosho katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI-Naliendele, mkoani Mtwara, ikiwa katika kitalu nyumba (Green House) kabla ya kupelekwa kwa wakulima.

> **"Kituo cha Ilonga – (Kilosa) Morogoro kimepewa jukumu la kuzalisha mbegu za alizeti, mtama, mahindi, mazao ya mikunde na mazao ya mizizi kama viazi vitamu kwa mikoa ya kanda ya kati," anasema bosi huyo wa Tari.**

Pia anaishukuru serikali, huku taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, kushiriki katika masuala ya kuzalisha mbegu na utoaji elimu ya mnyororo wa thamani ya mazao kwa wakulima, ili waweza kuzalisha kwa tija.

**MABOSI TARI KANDA**

Mkurugenzi wa Tari Ilonga mkoani Morogoro, Dk. Joel Meriyo, anasema mkakati wao ni kwamba mwaka huu wanalenga kuzalisha mbegu za alizeti za teknolojia ya kisasa kwa wastani wa tani 3000, zitakazosaidia kuzalisha alizeti zisizopungua tani 60,000 na kupunguza kasi ya uagizaji mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Dk. Meriyo anasema, Tari Ilonga kwa kushirikiana na vituo vyake vya utafiti vya Dakawa na Ifakara, mkoani Morogoro, katika msimu ujao wameweka mkakati wa kutafiti mbegu za mazao ya mkakati, kuzalisha na kuwauzia wakulima kwa bei wanayoimudu.

Anazitaja mbegu hizo za kisasa ni za mazao ya mkakati, ambayo ni mahindi, mtama, mpunga na mikundekunde, ambayo kimsingi inajumuisha maharage, mbaazi, dengu na choroko, lengo ni kuwahakikishia wakulima uwezekano wa kuanza kuzalisha malighafi ya viwanda kutoka shambani.

Anasema mbegu hizo zitakazoanza kuzalishwa zina uwezo wa kuhimili ukinzani na wadudu pamoja changamoto ya hali hewa, hali inayochangia uwezo wa kuwa na mazao hayo ya kimkakati.

Mkurugenzi huyo wa Ilonga, ambaye kitaaluma amebobea katika sayansi ya udongo, anasema ni mkakati unaonuia kujibu changamoto za wakulima, huku ikiunga mkono safari ya uchumi wa viwanda, kupitia upatikanaji malighafi.

Anasema, wakulima wana changamoto kama hali ya hewa na wadudu waharibifu, hivyo watafiti wa Tari wameamua kutafuta majibu ya kuwa na mbegu sahihi zinazokabiliana na changamoto zilizopo, ili kuwasaidia wakulima waongezea uzalishaji kupitia mazao ya kimkakati.

Meneja wa Tari Dakawa, wazalishaji mbegu bora za mpunga, Dk. Andrew Ngereza, anasema wameshatafiti mbegu bora ya mpunga ya teknolojia ya kisasa aina 'Saro 5 ' yenye uwezo wa kukabili wadudu na ukame.

Dk. Ngereza anataja kiwango cha uzalishaji inachomudu ni katika kila ekari moja mkulima, anapata mpunga kati ya magunia 35 mpaka 40 ya wastani wa kilo 90 hadi 100, tofauti na mbegu za kienyeji zinazotoa wastani wa gunia nane.

Anasema Tari Dakawa imetafiti na kuibua mbegu nyingine ya mpunga, yenye uwezo wa kuhimili maeneo yenye maji ya chumvi ambayo yamekuwa kikwazo kwa muda mrefu kwa wakulima wa mpunga.

Katika hilo Dk. Ngereza anawashauri wakulima kutumia mbegu hizo za teknolojia ya kisasa zenye uzalishaji mkubwa na rai yake ni wakulima waache mbegu za kienyeji.

Msimamizi wa Shamba la Msimba la Wakala wa Mbegu za Kilimo wilayani Kilosa, Jacob Chiwanga, anaasa wakulima nchini wabadilike kwa kuacha mbegu za kienyeji, kutokana na uhalisia wa tabianchi.

Anaeleza undani huo akitaja athari za kupungua kiwango cha mvua sasa, inaleta uhitaji tofauti wa zamani hatua na badala yake kutumia mbegu bora za teknolojia ya kisasa, ili kuzalisha malighafi ya kilimo yanayohitajika kwa uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi wa Tari Naliendele Mtwara, Dk. Fortunatus Kapinga, anasema wameshajipanga kuzalisha mbegu za korosho, zinazohimili magonjwa mbalimbali na kulifanya kuwa zao la kimkakati katika uchumi wa viwanda, kusaidia maeneo mapya yenye fursa ya kilimo hicho.

Anasema, upungufu wa mbegu za korosho na ufuta litakuwa historia, kutokana na kituo hicho kuongeza uzalishaji, baada ya kuanzisha mashamba mapya ya mbegu katika mikoa inayolima zao hilo kwa wingi, ikiwamo Tabora, Singida na Ruvuma kuwasaidia wakulima.

Mkurugenzi wa Tari Makutupora mkoani Dodoma, ambao ni watafiti wa zao la zabibu, Dk. Cornel Massawe, anasema wameshazalisha aina 86 za mbegu za zabibu kwa ajili ya kusaidia malighafi katika uchumi wa viwanda.

Anasema uzalishaji mbegu za zabibu zinazokinzana na wadudu zimefanyiwa majaribio katika maeneo tofauti ya mashamba ya wakulima na kuonyesha tija, huku katika baadhi ya maeneo wakulima wameshaanza uzalishaji wakitumia mbegu hizo za kisasa.

"Kutokana na uzalishaji wa mbegu hizo za kisasa umeifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili wa zao la zabibu katika nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa hiyo tuna imani tutakuza uchumi wa Viwanda," anasema Dk. Massawe.

Anasema, Mkoa Dodoma umekuwa mzalishaji mkubwa wa zabibu kitaifa na kimataifa, ikilimwa kwa wingi katika Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Dodoma (Jiji) na tayari kuna mikakati ya kugawa mbegu hizo za zabibu katika mikoa yenye fursa za uzalishaji wa zao hilo.

Kwa mujibu wa Dk. Massawe, anasema katika mkoa wa Dodoma, hivi sasa baadhi ya wakulima wamenzisha viwanda vidogo vya kusindika bidhaa hizo na wengine wanatengeneza mvinyo, kula kama matunda na utengenezaji pombe kali.

Mkurugenzi wa Tari Tengeru iliyopo Arusha, Dk. Stephano Sebastian, anasema wameshaweka mkakati wa kusaidia upungufu wa mbegu kwa mazao ya mboga na matunda, yanayotumika kama malighafi viwandani baada ya kupanua mashamba.

Dk. Sebastian anasema, upanuzi unajumuisha uzalishaji wa mazao kama parachichi, nyanya, sukuma wiki na mnafu.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, anasema wameshaipa jukumu Tari kuongeza uzalishaji mbegu bora za aina mbalimbali, ili kukidhi mahitaji ya wakulima na kufanya uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora.

Anasema, hiyo inaendana na uenezaji teknolojia rafiki ya uzalishaji na usindikaji mazao, ili kuongeza mnyororo wa thamani wenye yija na faida kwa wakulima nchini.

Mgumba anasema hadi sasa serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki, kwa kuhamasisha matumizi ya mbegu bora na utafiti unaonyesha kilimo kinachangia ukuaji haraka wa uchumi.

Kutokana na hilo, inaelezwa kuwa nyenzo inayochangia kupunguza umaskini kwa haraka kuliko sekta nyingine, kama ilivyoainishwa katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

Naibu Waziri anasema bado kilimo nchini kinakabiliwa na changamoto za matumizi madogo ya mbegu bora, mabadiliko ya tabia nchi, upungufu wa rutuba udongo, visumbufu vya mazao na zinginezo.

Katika kukabiliana na changamoto hizo hasa upatikanaji wa mbegu bora, Tari imeongezewa majukumu ya kushiriki kwenye uzalishaji wa mbegu, ili kukidhi mahitaji ya wakulima na kuongeza uhamasishaji wa matumizi ya mbegu kwa wakulima.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akikagua shamba darasa la korosho, katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tari-Naliendele, Mtwara, Desemba mwaka 2018. **PICHA ZOTE: WIZARA YA KILIMO.**

1, Tengeru: Mboga, matunda
2. Naliendele: Korosho, ufuta
3. Ilonga: Alizeti, mtama, mahindi
4. Dakawa/Ifakara: Mpunga, kunde
5. Makutupora: Zabibu....

## BIASHARA KATIKA PICHA



Wakazi wa Kijiji cha Bukumi, Musoma Vijijini mkoani Mara, Tanga Bugimbi aliyeshika plau na Majura Mbogora, wakilima shamba lao kwa jembe la kukokotwa na ng'ombe juzi, na pia wamekuwa wakikodishwa kulima mashamba ya watu wengine kwa Sh. 40,000 kwa kila heka moja.



Mkazi wa Kisaki mkoani Morogoro, Tunza Mgayuko (kushoto), akichangia mada ya kujadili matumizi ya nishati mbadala, katika mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wanawake kutoka mikoa mbalimbali.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Kanda ya Dar es Salaam, Hassan Athuman, akizungumza juzi kwenye hafla ya utoaji wa zawadi kwa wafanyakazi bora wa kiwanda cha mabomba ya Tanzania Steel Pipes (TSP), na kuhimiza nidhamu kazini. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

BIASHARA




Amani Sajila (aliyechuchumaa na kavaa shada la maua) akiwa kwenye picha ya pamoja na washiriki wenzake, baada ya kukabidhiwa gari lake.

# Simulizi za aliyepona kwa dawa asili, sasa muuzaji wake maarufu

- Ashinda Benzi droo ya kampuni mzalishaji
- Aweka kando nafaka, mtaji mpya mamilioni

**Na Beatrice Philemon**

AMANI Sajila ni mkazi wa Kimara Mavurunza, Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, anayefanya biashara kupitia mtandao wa mawasiliano, tangu Novemba 2016.

Akizungumza na Nipashe, Sajila anasema, mafanikio aliyopata katika biashara yalianzia na alipofanikiwa kutatua shida ya kiafya iliyomfika, kupitia kampuni ya Edmark Tanzania.

Sajila anasema, baada ya hapo ndipo akaanza biashara ya kuuza bidhaa tiba lishe na leo hii ni mshindi wa jumla wa gari aina ya Mercedes Benz katika shindano la kushindania gari lililowashirikisha wanachama zaidi ya 16,620.

Anasema, kabla alikuwa anasumbuliwa sana na ugonjwa wa mkojo mchafu au 'UTI sugu' na malaria kila mara na alikuwa anaugua mpaka na watu wahisi ana tatizo la kifafa.

Sambamba na hilo, Sajila anasema alisumbuliwa na alipoenda kupima afya katika zahanati mojawapo, aliambiwa ana 'UTI sugu' akaandikiwa dozi ya dawa za kutumia, lakini hakupata nafuu.

Anasema, ilhali anaendelea kuugua mwezi mzima na baada ya kuangaika sana, ndipo alipofahamishwa na kupelekwa na rafikiye kwa tabibu binafsi, kampuni ya Edmark inayozalisha bidhaa za tiba lishe.

"Nilipofika Edmark walinipima uzito na urefu ili kupata uwiano wangu wa uzito na urefu yaani ( Body Mass Index - BMI), waligundua nina uzito mkubwa wa kilo 99 ambao ulisababisha nijisikie kuwa mgonjwa sana," anasema.

Baadaye walimshauri kupunguza uzito usiozidi kilo 70 na kupangiwa dozi ya kupunguza uzito, kwa maana ya kupata uwiano sahihi wa tindikali na alkalaini mwilini, ambayo ni muhimu sana kiafya.

"Kikawaida alkalaini ambayo inatokana na maji, matunda na mbogamboga inatakiwa kuwa asilimia 80 mwilini na acid (tindikali) ni soda, baga, chipsi na vinywaji vyote na vyakula vya viwandani au visivyo vya asili inatakiwa kuwa asilimia 20," anasema.

Anafafanua kwamba, baada ya kutumia tiba aliyopangiwa, baada ya siku mbili tu alianza kuona mabadiliko chanya kimwili, akiyataja baadhi ya maeneo kama kiuno na mgongo, sehemu zilizomsumbua.

"Kulikuwa na aina mbalimbali za bidhaa za tiba kama vile; Shake Off, MRT, Splina, Café 73 na Troika ambazo nilikunywa," na anaongeza:

"Shake Off kwa ajili ya kusafisha tumbo, Meal Replacement Therapy (MRT) kwa ajili ya 'kubalance' uwiano wa acid (tindikali) na alkalaini na Edmark Gingseng Coffee kwa ajili ya kuyeyusha mafuta kwenye mishipa midogo.

"Mbali na hilo, kahawa ya Gingseng inasaidia pia kuongeza nguvu za kiume na hii inatengenezwa na mmea unaoitwa Gingseng kutoka Asia."

> **"Kikawaida alkalaini ambayo inatokana na maji, matunda na mbogamboga inatakiwa kuwa asilimia 80 mwilini na acid (tindikali) ni soda, baga, chipsi na vinywaji vyote na vyakula vya viwandani au visivyo vya asili inatakiwa kuwa asilimia 20," anasema.**

Anasema, baada ya kuzitumia, alipunguza kwa muda wa miezi miwili kwa uzito wa kilo 17 kutoka 99. 2 na maradhi yaliyomsibu yakatoweka.

**ALIVYOHAMIA BIASHARA**

Sajila anasimulia kwamba, tangu wakati huo aligeuka kuwa mpenzi wa bidhaa za kampuni anayofanyia biashara sasa na hata akaingia kwenye biashara yake.

Mshindi huyo anasimulia, baada ya hapo aligeuka kuwa mpenzi wa bidhaa hizo kabla ya kuingia rasmi kwenye udaku, akianza kwa kuwanunulia ndugu zake, kuonyesha marafiki na jamaa kuhusu bidhaa za Edmark.

Anasema, wengi walizipenda pamoja na ufafanuzi wa kina na misaada ya kuuipata. Hiyo ilikuwa mwaka 2017.

Hatua nyingine, anaitaja aligeuka kuwa mshauri wao wajiunge na kampuni ya Edmark, ili wazipate bidhaa hizo kwa bei nafuu na pia wafaidike na gawio (bonus) la Edmark kwa kila bidhaa wanayonunua wakiwa wanachama.

Anasema, baadaye wengi walikubali bidhaa hizo na wakajiunga na kampuni hiyo inayozalisha bidhaa za tiba lishe na mpaka sasa ameshaingiza wanachama 50, huku mwenyewe ni muuzaji wa bidhaa zao.

Sajila anasema, kadri muda ulivyosonga, alipata fursa za kuhudhuria semina za Edmark iliyomwongezea maarifa ya biashara na akajenga timu yake ya biashara, wakichangia pointi ambazo kwa mujibu wa mfumo uliopo, unawapa kiwango cha gawio za kuuza bidhaa.

Pia anasema mafunzo yamempatia ufahamu wa kujifunza mbinu za kibiashara, kuwasiliana na mteja, kanuni, sheria na taratibu za kampuni, uuzaji bidhaa kwa jumla, pia jinsi ya kuzijua na changamoto zake.

" Kwa kifupi 'system' (mfumo) ya mauzo katika kampuni ya Edmark ni rahisi sana, ukilinganisha na uuzaji wa bidhaa za kampuni nyingine zinazouza bidhaa kwa njia ya mtandao," anasema.

**MAFANIKIO YAKOJE?**

Kuhusu mafanikio aliyoyapata katika kampuni hiyo anayoitumika, Sajila anakiri ni makubwa, hasa anaporejea ushindi katika afya yake iliyotetereka mno kabla.

Pili, anagusa kipato chake kwamba kimeboreka sana akiwa na ziada, tofauti na miaka ya nyuma alikuwa katika kiwango cha chini, pasipo kutaja kiwango halisi.

"Kabla ya kujiunga na Edmark,



kipato changu kilikuwa kidogo. Nilikuwa nafanya biashara za mazao kama vile mahindi, mpunga, mchele. Wakati mwingine biashara hii ilikuwa inayumba kutokana na soko," anasema Sajila.

Anafafanua kuwa mara nyingi alinunua mazao kutoka kwa wakulima na baadaye anauza sokoni kwa bei ya jumla na kuna muda mtaji uliisha, kutokana na hali mbaya ya soko, pia hali ya hewa. Lingine analolifafanua ni kwamba, kampuni ya Edmark imemkomboa kwenye suala la muda, hivi sasa anasema ana fursa ya kufanya mengine ya ziada na inayomwongezea kipato.

Sajila anajivunia kwamba, uuzaji wa bidhaa tiba za lishe, zinasaidia mzunguko wake wa kifedha na mtaji wake umeongezeka akitaja umefika kiwango kikubwa zaidi.

"Bidhaa za tiba lishe za Edmark zinatoa matokeo halisi ya changamoto za kiafya, kisukari, pressure (msukumo damu), uvimbe, vidonda vya tumbo na kupunguza uzito, goita, 'Uric acid' na 'Constipation; yaani tatizo la kutopata choo na tatizo la kutopata siku kwa wanawake," anasema.

Katika nafasi ya kipekee, anataja faraja kubwa ya kununua gari aina ya Mercedes Benz Luxurious, kupitia droo iliyoshindanishwa na kampuni anayoitumikia kibiashara.

Anaelekeza shukurani zake kwa kampuni ya Edmark kuendesha kinyang'anyiro hicho nchini iliyo na fursa ya ushindi.

**NDOTO ZAKE**

Anasema, baada ya kufanikiwa kupata gari, inakuwa nyenzo kwake ya kupanua biashara yake, katika namna ya kurahisisha usambazaji bidhaa zake katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, aliko.

"Unajua ni ngumu sana kumwambia mtu njoo kwenye mafanikio kama wewe hujafanikiwa. Lakini, nikimwambia mtu njoo kwenye mafanikio, wakati huo akiona benzi, hana chakubisha... gari hii itanirahisishia na kufanya watu waniamini zaidi," anasema.

**MATATIZO YAKOJE?**

Kuhusu matatizo au vikwazo katika biashara yake, Sajila anasema kuaminika kwa mteja kwa mara ya kwanza huwa ni vugumu, hivyo inahitaji uvumilivu, roho ya upendo na huruma kumweleweshа mteja uhalisia.

Pia anasema ili mtu aelewe na kutumia bidhaa husika kwa manufaa ya kiafya, kuna mambo kama dhamana ya kwamba mteja anarudishiwa hela yake pindi atumiapo kama alivyoelekezwa na asipopata matokeo halisi.

Anasema, katika kufikia mafanikio hutumia nguzo kuu nne anazozitaja kuwa: Shukrani, Upendo, Utele na Huruma, jambo lililomwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali za kuwafikia wateja wa kiafya.

Miongoni mwa wateja wake ni wagonjwa wanaopatiwa tiba mbadala wa maradhi ya kitambi, kisukari, magonjwa ya ngozi kama vile chunusi, hata baadhi ya mahitaji ya kukabili athari za Ukimwi.

**VIJANA**

Anasema, kuna changamoto ya vijana kuchukua uamuzi na kuchangamkia fursa za biashara kama za Edmark, kwamba wengi ni wazito kuamini na inachukua hatua kuamini mbadala huo wa ajira, jambo linalowapotezea muda kushiriki umauzi mbele yao.

Ushauri wake wa sasa, ni vijana wachukue hatua, kwani fursa za kipato aina hiyo zipo na wakifika Edmark Tanzania, watapata mwongozo wa cha kufanya, ili mradi wana umri wa miaka 18 na ajue kusoma na kuandika.

> **"Kupitia mitandao hii, nimeweza kupata wateja wengi zaidi na wateja wengine kutoka Zambia, Afrika Kusini na hasa kwa bidhaa ya kupunguza uzito, ambayo ndiyo tatizo kubwa linalokabili dunia kwa sasa," anasimulia Sajila.**

Pia anaukumbusha umma kwamba, hivi sasa ni muda mwafaka wa kuzitafuta na kuzitumia bidhaa za tiba lishe, ili waweze kuboresha afya, pia kujiongezea kipato katika sura ya pili ya shilingi.

"Katika biashara zangu natumia zaidi mitandao ya kijamii kuuza bidhaa zangu za tiba lishe kama vile Face Book, WhatsApp na Instagram.

"Kupitia mitandao hii, nimeweza kupata wateja wengi zaidi na wateja wengine kutoka Zambia, Afrika Kusini na hasa kwa bidhaa ya kupunguza uzito, ambayo ndiyo tatizo kubwa linalokabili dunia kwa sasa," anasimulia Sajila.

**ALIVYOSHINDA GARI**

Anarejea usherehekeaji wa miaka saba ya Edmark Tanzania, alikwenda katika sherehe hiyo, lakini baadaye alitoka kwenda kurekodi nyimbo ya kwaya kuu Kinondoni Pale Victoria Studio na wakati yupo Studio aliondoa sauti.

"Baada ya kumaliza kurekodi na kuja kuwasha simu tu, nilikuta 'missed calls' zaidi ya 50 kutoka Edmark na ofisini. Muda si mrefu ikaingia tena simu ya dada Veronica Maganigani, nilipopokea tu, aliniambia moja kwa moja kwamba uko wapi? Umeshinda gari.

"Kwa kweli nilishikwa na kiwewe, kidogo nianguke, lakini Mungu huyu ninayemtumikia alinipa ujasiri, ulikuwa mshtuko mkubwa kwangu, sikuamini kama gari imekuja kwangu," anasema.

Anasema walipomaliza kurekodi, aliende penye sherehe na droo ilikofanyika, akikuta wenzake wakimsubiri na walipomuona, walishangilia mno.

"Namshukuru sana Mungu kwa rehema na neema zake, lakini nawashukuru sana Edmark kwa kutimiza ndoto zangu," anahitimisha.




Amani Sajila, akionyesha ufunguo wa gari baada ya kukabidhiwa. Pembeni yake ni washiriki wenzake wa shindano. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

UCHUMI

# Namna ya kukabili maisha kwa chaguo sahihi la nishati ya jikoni

## Mtaalamu: Tupunguze ‘bila mkaa mboga hainogi’

**Na Christina Mwakangale**

MATUMIZI ya nishati ya mkaa yanatajwa kuongezeka mara mbili zaidi, kwa kipindi cha miaka sita na kufikia tani milioni 2.3 kwa mwaka nchini, ikilinganishwa na mwaka 2010, yalikuwa tani milioni moja.

Hizo ni kwa mujibu wa takwimu za utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia, ulijikita katika kubaini matumizi ya nishati hiyo ambayo ni tegemezi kwa Watanzania wengi hususan mijini.

Mtaalamu wa Nishati ya Tungamo Taka na mabadiliko ya tabia nchi, Shima Sago anasema ipo haja kwa jamii kuondokana na dhana na mazoea ya kwamba kupika chakula pasipo mkaa, ladha huondoka.

“Mkaa mwaka 2010 ulitumika tani milioni moja pekee, lakini mwaka 2016 ulitumika tani milioni 2.3 kwa mwaka nchini, hii ni hatari kwa mazingira,” anasema Sago.

Mtaalamu huyo kutoka Taasisi ya Kuendeleza Teknolojia na Huduma ya Nishati Endelevu (TaTEDO), anayasema hayo jijini katika semina ya kuwajengea uwezo wanawake walioko ngazi za chini, ili watumie nishati mbadala kutoka mkoani Shinyanga, Morogoro na Dar es Salaam, iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Anasema taasisi hiyo kwa kushirikiana na Gamos kutoka Uingereza, ilifanya utafiti kubaini uwezekano wa kupika kwa umeme kwa kutumia umeme wa gridi ya taifa au wa jua (solar).

Anabainisha kuwa utafiti huo ulihusisha nchi ya Tanzania, Zambia, Myanmar na Kenya na ulilenga namna ya upikaji wa kawaida kwa kutumia gesi, mkaa, mafuta ya taa na kuni kwa kupika kwa kutumia umeme kwa wiki nne.

Mkurugenzi wa mtandao TGNP, Lilian Liundi, anasema lengo la semina hiyo ni kuwakutanisha wanajamii kutoka maeneo tofauti nchini, ili wabainishe changamoto zilizopo katika nishati pamoja na kuzitafutia ufumbuzi.

“Sio tu washiriki muibue changamoto mnazokumbana nazo bali tujadili namna ya kuzitatua kwa kutumia teknolojia rahisi na nafuu ya nishati mbadala,” anasema Liundi.

**WASHIRIKI JE?**

Mwezeshaji katika semina hiyo, mwanaharakati wa masuala ya kijinsia TGNP, Anna Sangai, anasema utafiti unaonyesha kuwa mwanamke wa Kiafrika anatumia saa 100 kwa mwaka, kwenda kutafuta kuni porini ili kupata nishati ya kupikia.

“Kuni ilitakiwa iwe historia, nishati jadidifu ni muhimu kwani ni vyanzo mbadala wa nishati isiyokwisha kwa mfano kinyesi, gesi, upepo na hata maporomoko ya maji,” anasema Sangai.

Anasema sera ya nishati bado haijatoa kipaumbele katika mwonekano wa kijinsia licha ya uwekezaji wa nishati jadidifu mpango wake kuwa ni Sh. bilioni 54.

“Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati unahitaji umeme na maji. Lengo namba saba la Mpango wa Maendeleo Endelevu (SGD’s 2030) unasema nishati mbadala kwa gharama nafuu ili kuhakikisha kila mtu anafikiwa na nishati,” anasema Sangai.



Nyenzo tofauti za mapishi, ambazo mustakabali wa matumizi yake uko katika utafiti na mijadala ya tija na uchumi wake. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

> **“Msimu wa masika debe la mkaa linauzwa Sh. 6,000 na wakati wa kiangazi linakuwa Sh. 1,000. Na bado kuna imani kwamba usipopikia chakula kwenye mkaa au kuni chakula hakiwi na ladha,” anasema Limbu.**

Kwangu Limbu, ni mshiriki wa semina anayesema matumizi ya mkaa katika kata ya Kiloleni, wilaya ya Kishapu ni ya kibiashara kutokana na wakazi wa eneo hilo kuhifadhi magunia kwenye maghala kwa wingi hususan msimu wa kiangazi.

“Msimu wa masika debe la mkaa linauzwa Sh. 6,000 na wakati wa kiangazi linakuwa Sh. 1,000. Na bado kuna imani kwamba usipopikia chakula kwenye mkaa au kuni chakula hakiwi na ladha,” anasema Limbu.

**YA UTAFITI**

Mtaalamu Sago, anasema utafiti uliofanywa na Tatedo ulilenga kuangalia muda gani unatumika katika kupika chakula, jinsi ya kupika na kiasi cha nishati kinachotumika pamoja na kila nyumba aina ya utamaduni inaoutumia katika kupika.

Anasema matokeo ya utafiti na sababu zake, ilikuwa kufahamu kwa namna matumizi ya nishati na gharama zake, aina ya nishati, chakula, vifaa vya kupikia, namna ya upikaji na idadi ya walaji.

“Utafiti ulilenga maswali haya, je, kupika kwa gesi au mkaa ni ghali ukilinganisha na kupika kwa umeme? Lakini inaonyesha kupika kwa umeme ni chini ya uniti mbili iwapo una vifaa sanifu vya kupikia kama ‘pressure cooker’, ‘rice cooker’, ambazo bei yake ni sawa na Sh. 730.

“Mazoea ya kupika na umeme yanaweza kuwa kichocheo kikubwa katika matumizi bora na sanifu ya nishati ya umeme itapunguza matumizi hadi uniti moja kwa siku,” anasema Sago.

Sagi anaaleza wastani wa gharama ya kupika kwa kutumia umeme ni Sh. 21,900 kwa mwezi, huku mtungi wa gesi unaouzwa Sh. 45,000 na gunia la mkaa ni kati Sh. 50,000 hadi Sh. 80,000 kwa mwezi kwa mkazi wa jijini Dar es Salaam.

Anasema iwapo nishati ya umeme ikitumika kwa ajili ya kupika itapunguza uchafuzi wa mazingira, itaboresha afya na kupunguza gharama ikiwamo kuboresha usafi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuja na kushoka inayojihusisha na utengenezaji mkaa mbadala kwa kutumia taka zinazoteketezwa, Leonard Kushoka, anasema asilimia 60 ya taka zilizokuwa zinateketezwa jijini Dar es Salaam, ikiwamo za majani zinaweza kutumika kwa ajili ya kutengenezea mkaa mbadala.

Anasema zaidi ya tani 5,000 za taka zinazozalishwa jijini Dar es Salaam kila siku kati ya hizo asilimia 40 zinaoza na asilimia 60 huteketezwa.

Anasema asilimia 50 ya mkaa unaotokana na kuchoma miti nchini, unatumika jijini Dar es Salaam na kusababisha uharibifu wa misitu unaochangia ongezeko la mabadiliko ya tabianchi.

“Mkaa mbadala ndio suluhisho kwa mabadiliko ya tabianchi, asilimia 95 ya Watanzania wanatumia mkaa utokanao na kuni, hii inatokana na ukosefu wa fedha kwamba hawamudu kutumia gesi, umeme,” anasema Kushoka.

Anaeleza kwamba taka ambazo zinazalishwa katika miji mikubwa ikiwamo Arusha, Mwanza na Mbeya zinaweza kuajiri vijana kupitia viwanda vidogo.

“Mkaa huu kwa kutumia mashine maalum unaweza kuzalisha gunia 20 hadi 50, kilo mbili ya mkaa mbadala huuzwa kati ya Sh. 5,000 na unadumu kwa muda mrefu.”







Mafundi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wakihangaika kukata umeme katika eneo la Kiwira, baada ya gari la mchanga kugonga pikipiki na kuangukia kwenye nguzo ya umeme. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Polisi wamaliza utata wa jeneza lililokutwa sokoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limekamilisha uchunguzi wa tukio la jeneza lililokuwa linadaiwa kutelekezwa katika Soko la Soweto jijini Mbeya, likiwatoa hofu wananchi kuwa tukio hilo halihusiani na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, jana aliwaambia wandishi wa habari jijini hapa kwamba, baada ya kufanya uchunguzi wa kina, jeshi hilo lilibaini jeneza hilo liliachwa kimakosa sokoni hapo. Alidai kuwa awali muumini wa dini ya Kiislamu, Masoud Mohamed, aliyekuwa mfanyabiashara wa Mji wa Makambako mkoani Njombe, alikuwa anauguzwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na alifariki dunia na kifo cha kikawa chanzo cha tukio hilo.

Alidai ndugu wa marehemu waliamua kusafirisha mwili wa ndugu yao huyo kwenda kuzika mkoani Njombe na hivyo wakaamua kwenda kuazima jeneza hilo katika Msikiti wa Masjid Taufiq uliopo Block Q, eneo la Soweto jijini hapa.

Aliendelea kueleza kuwa wenye msikiti huo, waliwapatia wanafamilia hao jeneza hilo kwa masharti kuwa wakishakamilisha shughuli za mazishi, wanatakiwa kulirejesha kwa ajili ya matumizi ya msikiti huo. Alidai kuwa baada ya shughuli za mazishi kumalizika huko Makambako, mmoja wa wanafamilia hao alipewa jukumu la kutafuta usafiri wa kusafirisha jeneza hilo kulirejesha Mbeya na akapata gari ya mizigo aina ya Fuso lililokuwa likipeleka nyanya katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Kamanda huyo alidai walipopakia jeneza hilo kwenye hilo gari walimpatia dereva wake namba za simu ya mtu aliyepaswa kupokea jeneza hilo mjini Mbeya, akimtaja kuwa kuwa Hamis Hamad, ambaye ni mfanyakazi wa msikiti huo.

Alidai kwa bahati mbaya, dereva wa gari hilo alifika Mbeya usiku na kwenda moja kwa moja katika Soko la Soweto kushusha nyanya zilizotakiwa kushushwa Mbeya na baadaye aendelee na safari ya kwenda kupeleka mzigo mwingine wa nyanya mkoani Songwe.

Kamanda Matei alifafanua kuwa alipofika katika Soko la Soweto, alijaribu kumpigia simu mhusika aliyepaswa kupokea jeneza hilo, lakini kwa bahati mbaya simu hiyo haikupatikana na ndipo dereva alipowaomba walinzi wa Soko la Soweto aliache jeneza hilo ili asubuhi wampigie simu mhusika aliyepaswa kulichukua.

"Hata hivyo, ilipofika asubuhi, bado yule mtu aliyetakiwa kufika kuchukua jeneza alikuwa hapatikani kwenye simu na muda wa walinzi kuendelea kubaki sokoni hapo ulikuwa umemalizika na ndipo na wao wakaondoka bila kumkabidhi mtu yoyote.

"Hali hiyo ilisababisha taharuki kwa wananchi waliowahi sokoni na kukuta jeneza hilo likiwa halina maelezo yoyote," Kamanda Matei alisimulia.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, Jeshi la Polisi lilimkamata mlinzi aliyekabidhiwa jeneza hilo ili kupata maelezo ya kina na kwamba mlinzi huyo alisaidia kuwapata wahusika ambao pia wamehojiwa na jeshi hilo na kujiridhisha kuwa hapakuwapo na kosa la jinai kwenye tukio hilo.

Aliwataka wafanyabiashara wa soko hilo kuendelea na shughuli zao bila kuwa na wasiwasi juu ya tukio hilo na akawataka kuepuka kuyahusika matukio mbalimbali na imani za kishirikina.

# Chuo chawezeshwa vifaa kuongeza ubunifu

**NA Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imekabidhi seti 20 za kompyuta kwa Chuo cha Mafunzo ya Ujenzi wa Mindombinu ya Barabara wilayani Rungwe ili kuongeza ubunifu na ufanisi wa mafunzo kwa wanafunzi wa chuo hicho.

Kompyuta hizo zilikabidhiwa chuoni hapo na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Zaina Mlawa, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo.

Zaina aliutaka uongozi wa chuo hicho kuzitumia kompyuta hizo kwa uangalifu na ziwe chachu ya utendaji wa kazi kwa ufanisi chuoni hapo.

"Kwan niaba ya Katibu Mkuu, nawakabidhi kompyuta hizi 20 kama mlivyoomba na ni matarajio yetu kuwa mtazitumia vizuri ili ziwe chachu ya kuboresha utendaji kazi na kuleta mabadiliko chanya kwenye taasisi yenu," alisema. Akipokea msaada huo, Mkuu wa Chuo hicho, Mahmoud Chamle, aliishukuru wizara kwa kukikumbuka chuo hicho, akieleza kuwa chuo chake ni miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo.

Alisema uongozi wake unaamini vifaa hivyo vitachochea mabadiliko chanya ya utendaji kazi wao.

Mchale alisema kompyuta hizo zimekuja muda mwafaka kwa kuwa kuna kazi nyingi zilikuwa zinahitaji vifaa hivyo na kazi mojawapo ni kufundisha programu za uchoraji na ujenzi wa barabara.

"Kama nilivyosema awali, ni kwamba kompyuta hizi zina matumizi mengi ikiwa ni pamoja na kufundishia programu zinazohusiana na ujenzi, hasa uchoraji wa barabara," alisema.

Chamle alisema kompyuta hizo ni mwanzo mpya wa chuo hicho kufanya kazi kisasa na wanakusudia kuanzisha mtaala mpya wa kuchora michoro ya ujenzi wa barabara na miundombinu mingine, hivyo zitaongeza uwezo wa chuo kufanya kazi kwa weledi.

## Wafanyabiashara walalamika lugha chafu maofisa wa TRA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA mkoani Mbeya wamelalamikia maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuwa wanawatolea lugha chafu na vitisho vinavyokuwa kikwazo kwao kulipa kodi kwa hiari.

Wakizungumza mbele ya Mkurugenzi wa Idara ya Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, wafanyabiashara hao walimdai baadhi ya maofisa wa mamlaka hiyo mkoani Mbeya, wamekuwa wakitumia lugha kali kuwalazimisha kulipa kodi.

Walidai baadhi yao pia hawana ushirikiano kwa wafanyabiashara katika kutoa elimu kwa mlipakodi na kila kunapokuwa na kosa, hukimbilia kutoza faini bila kuwapa fursa ya kujitetea.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika maeneo ya Kabwe na Sido jijini Mbeya, Emmanuel Ndakam, alisema kauli za vitisho zimekuwa zikijenga ukuta na kuweka uadui kati ya wafanyabiashara na watumishi wa TRA, hali ambayo inakwamisha suala ulipaji kodi kwa hiari.

Ndaka aliuomba uongozi wa juu wa TRA kuwaelimisha watumishi wake ili kujenga uhusiano mzuri na wafanyabiashara kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Alisema wafanyabiashara walio wengi, hawana uelewa na elimu ya kutosha kuhusiana na masuala ya kodi, hivyo bado wanahitaji elimu badala ya kupigwa adhabu kila wakati.

Alitoa mfano kuwa suala la wafanyabiashara kuandaa taarifa za biashara zao pamoja na elimu ya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ni tatizo kwa wafanyabiashara walio wengi, hivyo wanahitaji kupewa elimu.

"Baadhi ya watumishi wa TRA ni kikwazo kwa wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari, mfanyabiashara anaweza kufanya kosa mfano kwenye suala la utoaji wa risiti, pengine kwa mashine ya EFD kukorofisha, badala ya ofisa wa TRA kumwelimisha, yeye anamtolea lugha za vitisho," alilalamika.

Edmund Msaki, mfanyabiashara katika eneo la Kabwe jijini hapa, alisema ziara ya mkurugenzi huyo kutoka makao makuu ya TRA inaonyesha wazi kuwa viongozi wa ngazi ya juu hawana tatizo, bali watendaji wao wa chini.

Alisema ujio wa kiongozi huyo wa ngazi ya juu utasaidia kuwapunguzia hofu wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya ambao wakati wote wamekuwa wakiona TRA kama maadui.

Akijibu hoja za wafanyabiashara hao, Kayombo, aliyeongozana na maofisa wengine kutoka TRA Mkoa wa Mbeya, alisema lengo la kuwatembelea wafanyabiashara hao ni kutoa elimu na kusikiliza vikwazo vinavyowakabili.

Mkurugenzi huyo pia alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wafanyabiashara umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati.

Kayombo alisema wamekuwa wakiwapa elimu watumishi wa TRA namna ya kuwahudumia wateja na wamekuwa wakichukua hatua na kinidhamu dhidi ya walioonekana kwenda kinyume cha maadili.

"Lengo la ziara yetu ni kuwaona wafanyabiashara ili kusikiliza kero zenu, lakini kutoa elimu kuhusiana na masuala ya kodi na kuwakumbusha kulipa kodi kwa wakati pamoja na umuhimu wa kutoa risiti kwa wateja mnaowahudumia," alisema.





# Serikali yaahidi mazingira rafiki uwekezaji, biashara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wote wa maendeleo ambao wanawekeza nchini ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira rafiki kwao.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, alisema hayo juzi alipokuwa akizindua pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi katika kituo cha mafuta cha Admire Oil.

Mavunde alisema serikali inathamini wawekezaji kutokana na mchango wao katika kutoa ajira na kukuza pato la Taifa kupitia kodi wanazolipa.

"Niupongeze uongozi wa kampuni hii kwa kuona umuhimu na ulazima wa kuja kuwekeza katika Jiji la Dodoma kwani kufanya hivyo kutaongeza fursa kubwa za ajira kwa vijana ikizingatiwa tayari mmeshaajiri watu 20 mpaka sasa kwa wakazi wa Dodoma," alisema.

"Serikali tunaendelea kutoa wito kwa wawekezaji wengine kuja kuwekeza Dodoma ambako ni makao makuu ya serikali, lakini kuna maeneo mengi ya uwekezaji na rafiki kwa ajili ya kujenga viwanda, hoteli na hata majengo ya kibiashara," alisema Mavunde. Awali, Msemaji wa Admire Oil, Mohamed Ibrahim, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji jambo ambalo linaongeza ari kwao ya kuzidi kufanya uwekezaji katika maeneo mengi nchini.

"Kwa kweli serikali ya Rais (John) Magufuli imetoa mazingira rafiki sana kwa wafanyabiashara hasa wazalendo. Sisi tunaahidi kuendelea kushirikiana na serikali yetu ili kufikia ndoto ya Rais ya viwanda," alisema.

"Tunafahamu lengo la kila mfanyabiashara ni kuwekeza na kupata faida lakini kampuni yetu ya Admire moja kati ya malengo yake makubwa ni kugawa ajira kwa kinamama na vijana wengi nchini," alisema Ibrahim.

Aidha, alisema wameajiri vijana takribani 150 nchini na kati ya hao wengi ni wanawake ili kuwainua pamoja na kuwawezesha kiuchumi.

Pia alisema Admire Oil ina matawi mengi katika mikoa mbalimbali nchini kituo kikubwa kikiwa ni mkoa wa Pwani pamoja na mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na D



Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Jiji la Dodoma, Sharifa Balaganya, akizungumza wakati akifungua mkutano wa kuunda mtandao wa vikundi vya vijana (hawapo pichani), uliofanyika jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Mbunge ataka tume huru uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda (Chadema), amewaomba Watanzania kuungana kudai tume huru ya uchaguzi.

Akizungumza jana jijini hapa, Mwakagenda alisema, mwaka huu ambao ni mwaka wa uchaguzi kuna haja ya kuwa na tume huru ya uchaguzi ambayo itatatua changamoto ambazo zimekuwa zijitokeza katika uchaguzi mbalimbali.

"Naomba Watanzania tuungane kwa umoja wetu bila kujali itikadi ya vyama vyetu ili tudai tume huru ya uchaguzi sambamba na wanawake wengi wajitokeze kugombea na kupiga kura," alisema Mwakagenda.

Pia aliwataka wanawake wa chama hicho kutumia fursa ya kugombea nafasi mbalimbali ndani ya serikali kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Aidha, alisema kuwa wanawake wanatakiwa kuingia katika mwaka 2020 kwa malengo chanya tofauti na ilivyo mwaka uliopita.

Ikiwa ni sehemu ya salamu ya mwaka mpya kwa wanawake wa Chadema na nje ya chama hicho, Mwakagenda alisema kwamba wanawake wanatakiwa kubadili mtazamo wa kujitosa katika shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

"Mwaka 2020 uwe mwaka wa mabadiliko wanaweke kwa sasa wanatakiwa kubadilika na kubadilisha mtazamo, badala ya kuwaza kubebwa wanatakiwa kuonesha uwezo wao na utayari wa kufanya mambo," alisema.

"Imekuwapo mitazamo ya kuwa nafasi ya mwanamke ni kuwa katika ngazi za chini. Mfano mzuri ni katika mwaka huu wa uchaguzi mkuu, wanawake wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali ambazo wanaona zinawafaa," alisema Mwakagenda.

# Takukuru yatuma salamu uchaguzi 2020

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma imewaonya wagombea nafasi mbalimbali kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Onyo hilo limekuja siku chache baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, kuiagiza Takukuru kuweka nguvu katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akizungumza na waandishi jana, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wamejipanga kila kona kuhakikisha uchaguzi mkuu ujao unakwenda salama na wanapatikana viongozi ambao wana uwezo wa kuongoza ikiwamo kusimamia miradi ya maendeleo.

"Naomba wanaogombea katika uchaguzi mkuu wajinadi kwa sera na si kutegemea kutoa rushwa kwa wananchi ili wapite kirahisi. Wakifanya hivyo wataishia mikononi mwa dola," alisema Kibwengo.

Alisema Takukuru imejipanga kuhakikisha uchaguzi huo unafanikiwa asilimia zote kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana.

Kibwengo alisema Takukuru imejiimarisha kama walivyoagizwa kutekeleza majukumu yao ya kuangalia uchaguzi kuhakikisha unakwenda salama bila rushwa.

Kutokana na hilo, alisema wana kila sababu ya kuweka mitego kila kona ya mkoa ambako uchaguzi huo utakuwa umepangwa kufanyika.

Mbali na hilo, aliwataka wananchi katika maeneo mbalimbali kutokubali kurubuniwa na wagombea ili wawachague kirahisi katika nafasi mbalimbali wanazowania. Kibwengo alisema wananchi hawana sababu ya kubabaika wanachotakiwa ni kuangalia mtu sahihi ambaye ataleta manufaa katika kata anayoiongoza.

"Wananchi tumieni haki yenu kuchagua watu wanaopenda maendeleo. Kumbuka mkikubali kupokea rushwa na wewe utakuwa hatiani kwa sababu sheria inasema mtoa rushwa na mpokea rushwa wote wana makosa," alisema Kibwengo.

Alifafanua kuwa kinachotakiwa ni kila mmoja atumie akili kuangalia kiongozi gani anafaa kwa ajili ya kuongoza eneo analotakiwa kuliongoza katika miaka mitano.



# Shein afagilia sekta binafsi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema sekta binafsi ikiwamo biashara, zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya mataifa mbalimbali duniani.

Dk. Shein alisema hayo jana katika ufunguzi wa jengo jipya la Shule ya Sekondari ya Biashara iliyoko Mombasa mjini Zanzibar.

Alisema mwaka 1980 Serikali ya Zanzibar iliondokana na mfumo wa kuhodhi biashara na badala yake kujikita katika usimamizi wa sera na sheria ili kutoa fursa kwa wadau wa sekta hiyo kufanya shughuli hizo kwa upana.

"Watu wa sekta binfasi ikiwamo biashara ndio wanaoimarisha nchi zao duniani kote. Serikali haiwezi ikafanya kila kitu," alisema.

Rais pia alisema hatua ya wafanyabiashara kurejesha faida kwa wananchi, hususan wanyonge, huleta baraka kubwa, akinasibisha kauli hiyo na hatua ya mfanyabiashara Ahmada Yahya Abdulwakil aliyefadhili ujenzi wa jengo la shule hiyo na kusema ni miongoni mwa wafanyabiashara weledi na wanaofanya vyema.

Alisema anawaheshimu wafanyabiashara wakiwamo wale wanaofanya vyema shughuli zao kwa uadilifu na kurejesha faida kwa jamii.

Pia alisema kuna umuhimu wa kuwaendeleza vyema wanafunzi wa shule hiyo juu ya namna bora ya kufanya biashara ili kulisaidia taifa na kwamba taifa linahitaji wataalamu wa kutosha katika masuala ya uchumi.

"Uzinduzi wa shule hii ulete tija kubwa baadaye kwa kutoa wataalamu wengi zaidi wa uchumi," alisema.

Aidha, Dk. Shein alisema mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya elimu nchini, kuanzia mwaka 1964 hadi sasa, yanalenga kuifikisha Zanzibar katika maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, Zanzibar ni miongoni mwa nchi chache duniani zenye mfumo wa kutoa elimu bure, huku ikilenga kupanua wigo wa hatua hiyo hadi kufikia ngazi za chuo kikuu pale uchumi wake utakapoimarika.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, elimu ilihodhiwa na wakoloni ambapo ni wazalendo wachache wenye uwezo ndio waliopata fursa ya kusoma na kuliacha kundi kubwa la wazalendo bila kupata fursa hiyo.

Naye Abdulwakili, ambaye ni Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, alisema kwa kushirikiana na serikali amefanikisha dhamira ya ujenzi wa jengo hilo, ili kusaidia juhudi za kuondokana na uhaba wa madarasa unaozikabili shule mbalimbali na kuwafanya wanafunzi kusoma katika mazingira bora.

Alimshukuru Dk. Shein kwa kubainisha umuhimu wa wananchi wakiwamo wafanyabiashara kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idris Muslim, alisema ujenzi wa jengo hilo la ghorofa mbili, likiwa na madarasa tisa na ofisi mbalimbali za huduma za kitaaluma, umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.1 hadi kukamilika kwake.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kutaondoa mrundikano wa wanafunzi katika madarasa, kutoka wanafunzi 49 kwa darasa hadi kufikia 36 kupitia mkondo mmoja wa masomo.

## Waziri ahimiza usafi mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, amewataka wananchi kuendeleza kudumisha usafi wa mazingira ili kuondokana na maradhi.

Aliyasema hayo jana baada ya kumalizika kwa usafi katika eneo la Kituo cha Afya kwa Wazee, Sebleni, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema afya ni muhimu kwa kila mtu na wizara imeona kuna haja ya kufanya usafi katika kituo hicho na kuongeza kuwa huduma za afya zinahitaji kuboreshwa kituoni hapo kutokana na changamoto zilizopo.

"Zaidi ya usafi wa majani na mwitu, kituo chenyewe ni kikubwa kwa eneo hili, hivyo kinahitaji kuboreshwa kwa kuwa imara na kuendeleza uwezo wa kuwapatia huduma zaidi wananchi wanaofika kituoni," alisema.

Alisema wizara yake imeshaanza kufanya matengenezo ya kujenga ukuta sehemu ya kinamama wanaofika kujifungua ili kutengenisha na kuweka furaha ya wamama wanaokwenda kupatia huduma katika kituo hicho.

Pia alisema wamewatatulia changamoto ya huduma ya maji kwa kurejesha mfumo wa maji na mabomba.

Naye daktari wa kituo hicho, Khamis Hassan Said, alisema wanaishukuru serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuona umuhimu wa kwenda kufanya usafi na kuonyesha moyo wa kuwajali.



Rais mstaafu wa Awamu ya Sita, Dk. Aman Abeid Karume, akikata utepe katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa jengo jipya la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Malindi (MOTOR TRADE) Zanzibar. Ikiwa ni shamra shamra za miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMA**

# Karume asema ongezeko la benki ishara ukuaji uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, amesema kuongezeka kwa matawi ya huduma kwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni ishara nzuri ya kukua kwa uchumi Zanzibar.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza katika sherehe ya uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la benki hiyo, huko Malindi Unguja ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya kutimiza miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Karume alisema kuimarisha shughuli za kibenki kwa kutumia njia za kiteknolojia kutawarahisishia wateja kupata huduma kwa haraka.

Alisema hatua ya serikali kujenga matawi mbalimbali ya huduma za kibenki, itasaidia kuepusha msongamano wa wateja na kuwarahisishia wateja kupata huduma zao kwa haraka na kwa wakati.

Kwa mujibu wa Karume, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ikitumia benki hiyo kwa ajili ya shughuli za kiserikali, lakini baada ya kuona benki nyingi zinabinafsishwa, ikaanzishwa Benki ya Watu wa Zanzibar ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wake.

Aliwataka wafanyakazi wa benki hiyo kuwa makini katika utekelezaji wa kazi zao kwani kufanya hivyo kutasaidia kuepusha migogoro kwa wateja.

Hata hivyo, aliwataka wateja ambao wanapatiwa mikopo kulipa kwa wakati na utaratibu uliopangwa ili na wateja wengine waweze kupata kuduma hiyo .

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema ongezeko la kiwango kikubwa cha gawio na kodi ya mapato katika huduma za kibenki kutaimarisha ukuaji wa uchumi kwa haraka.

Alisema lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia maendeleo wananchi wake na kuwapunguzia makali ya maisha kwa njia ya mikopo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Juma Ameir Hafidh, alisema, kukamilika kwa jengo hilo, kutaweza kukidhi mahitaji ya kibenki kwa wakati wa sasa na baadaye.

Pia alisema utayarishaji wa michoro na usimamizi wa ujenzi huo unafanywa na mshauri elekezi ambaye ni kampuni ya NEDCO kutoka Dar es Salaam.

Alisema ujenzi huo ulichelewa kutokana na kutopatikana kwa mchanga na mawe katika ujenzi, taratibu ndefu za upatikanaji vibali katika kila hatua ya ujenzi katika maeneo ya hifadhi ya Mji Mkongwe.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa ujenzi wa jengo hilo, unatarajiwa kumalizika Aprili, mwaka huu.

# Askofu aonya wanasiasa vurugu uchaguzi mkuu

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

ASKOFU wa Kanisa la International Evengelical Assembles of God (IEAGT) Shinyanga, David Mabushi, amevitaka vyama vya siasa kulinda amani wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu mwaka huu.

Alitoa wito huo juzi kwenye ibada maalum ya kuiombea nchi amani na utulivu, kuelekea kipindi cha Uchaguzi Mkuu na kumwombea Rais John Magufuli ili aendelee kuchapa kazi.

Alisema kipindi cha uchaguzi huwa na viashiria vingi vya uvunjifu wa amani, hivyo kuna haja vyama vya siasa kuheshimu sheria za uchaguzi na katiba ya nchi, ili kuendelea kuilinda amani iliyoasisi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

"Naviomba sana vyama vyote vya siasa hapa nchini, kuheshimu sheria za uchaguzi na katiba ya nchini, ili uchaguzi mkuu ambao unafanyika mwaka huu wa kuchagua madiwani, wabunge na Rais, ufanyike kwa amani na utulivu.]

"Hata kwenye vitabu vya Mungu ukisoma Biblia, maandiko yanasema kila mtu anapaswa kutii mamlaka ya utawala na sheria zilizowekwa, sasa wewe ukienda kinyume, utakumbana na hukumu ya Mungu, kwa sababu utawala umewekwa na Mungu ili kulinda amani," alionya. Alisema anamwombea Rais Magufuli kwa Mungu aendelee kuwa na afya njema na hekima ya kuiongoza nchi kwa ari ileile ya kuliletea taifa maendeleo.

Alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kimaendeleo chini ya uongozi wake, hasa katika miundombinu ya barabara, vituo vya afya, miradi ya maji, umeme na usafiri wa anga.



Wakazi wa vijiji vya Mkumbululu na Luatala Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wakipita ndani ya maji katika Mto Mkoo uliopo Kata ya Mchaulu baada ya daraja linalounganisha vijiji vyao kukatika juzi kutokana na mvua. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Serikali yapewa neno ufugaji nyuki

**Na Julieth Mkireri,**

KIBAHA

MTAFITI wa Misitu, Ibrahim Hussein, ameishauri serikali kutoa kipaumbele kuhamasisha jamii kufuga nyuki, ili kuongeza kipato na kuzalisha asali bora itakayouzwa ndani na nje ya nchi.

Alitoa rai hiyo alipozungumza na waandishi wa habari, baada ya mafunzo ya ufugaji nyuki yaliyofanyika mwishoni kwa wiki mjini Kibaha. Katika mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Kuhifadhi Mazingira la Kibaha Nature Conservation Initiative na kushirikisha washiriki zaidi ya 40 kutoka vikundi vya Twikinde cha Pangani, Wazee Bamba na Mwambisi vya Kongowe, Pwani.

Ibrahim alisema ufugaji nyuki unatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwa ni moja ya shughuli ambazo zina nafasi kubwa ya kuinua watu kiuchumi. Alisema wanufaika wa mafunzo hayo watakapoanza ufugaji, watapatiwa mafunzo ya ubora kutoka kwa mtaalamu wa Shirika la Viwango (TBS), ili asali yao iuzike ndani na nje ya nchi.

"Tunatakiwa kuwaunga mkono kwenye malengo ya kufuga asali, nimeamua kutoa mizinga hii 40 ili baada ya mafunzo hayo waanze kufuga na kujipatia kipato," alisema.

Ibrahim alisema ipo mizinga mingine ambayo ameitoa kwa watu binafsi ili kufuga nyuki na kuondokana na umaskini. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kibaha Mjini, Edwin Shunda, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya jumuiya hiyo ngazi ya taifa. Shunda alisema mafunzo hayo yatawawezesha washiriki kufuga kisasa na kupata asali iliyo bora ambayo wataiuza maeneo mbalimbali na kujipatia kipato.

Alisema vikundi hivyo kila kimoja vimepata mizinga mitano ambapo Jumuiya ya Wazazi Kibaha Mjini imepatiwa mizinga 25.

## Vituo vya afya 73 nchini vyafungiwa

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imezifungia hospitali 72 kutoa huduma ya mionzi katika mikoa 23 ya Tanzania Bara na Visiwani. Hospitali hizo zimefungiwa kutokana na kukiuka masharti ya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003 juu ya utoaji wa huduma ya mionzi.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TAEC, Peter Ngamilo, alisema jana kuwa tume imefikia hatua hiyo baada ya ukaguzi uliofanyika kwa nyakati tofauti mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi uliopita.

Ngamilo alitaja baadhi ya sababu zilizofanya kusitisha huduma katika hospitali hizo kuwa ni kukosa wataalamu (wanaradiolojia) wa kutoa huduma za mionzi, ubovu wa mashine za mionzi (X-Ray, CT- Scan na Radio theraph), kukosa leseni ya utoaji wa huduma na kukosa alama za tahadhari kuashiria huduma ya mionzi ikiwa inaendelea.

"Hatuwezi kufanya mchezo na afya za binadamu. Lazima ukaguzi wa uhakika ufanyike na ukaguzi huo unafanyika mara mbili kwa mwaka ndiyo maana tumebaini changamoto za vituo hivyo nchini kote, hivyo tumevisitishia huduma.

"Kituo chochote kitakachotimiza masharti kitatuandikia barua nasisi tutakwenda kukagua kama masharti yamefikiwa ili kuruhusu kuendelea na utoaji wa huduma," alisema Ngamilo.

Ngamilo alivitaja vituo hivyo kuwa ni Kituo cha Afya Kaloleni, Kituo cha Afya Kansay, Hospitali Teule ya Wilaya ya Karatu, Kituo cha Afya Mong'ola, Al-Hilal Polyclinic, Kituo cha Afya Magomeni (Kitengo cha Meno) na Hospitali Mnazi Mmoja (Kitengo cha Meno).

Vingine ni Mselemu Medical Health, Hospitali ya Mwananyamala Kitengo cha Meno, Kituo cha Afya Mama Ngoma, Kituo cha Afya Sinza (Kitengo cha Meno), Zahanati ya Magereza – Ukonga , St. Bernard Charitable, Skol Building Contractor, Sinza Africa Sana, Dar Health, Centre na Al-Jumaa Charitable Dispensary.

Pia vimo Kinondoni Municipal – Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP) – Tarura, Kigamboni Health Centre (kimefungwa kwa muda), China Railways Seventh Group, Mlali Rehabilitation Centre na Hospitali ya Lutheran Ilula.

Mkuu huyo alitaja vituo vingine kuwa Kituo cha Afya Izimbya, Hospitali za Ndolage, Nyakaiga, Mugana, Ufufuo, Matyazo, Bwambo, Gonja, Kilimanjaro Health Centre, Papri Medical Centre (Moshi), Regional Dermatology Centre, Same , St. Joseph Uchira Dispendary, Usangi Rondo na Hospitali ya Rufani ya Sokoine Lindi.

Vingine ni vituo vya Afya Balang'dalalu, Gendabi, Hospitali ya Misheni Kibara, Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Hospitali ya Kilutheri Matema na Hospitali ya Wilaya Mbarali.

HABARI KIMATAIFA

# Netanyahu aomba kinga bunge kuepuka mashtaka

**Tel Aviv, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, ameamua kutafuta kinga ya bunge dhidi ya mashtaka ya ufisadi yanayomkabili.

Hatua hiyo huenda ikachelewesha kesi dhidi yake hadi uchaguzi utakapofanyika mwezi Machi.

Waziri Mkuu huyo alishtakiwa na mwanasheria mkuu kwa makosa ya kutoa hongo, kufanya udanganyifu na kuwavunja imani raia waliomchagua kuhusiana na kesi tatu tofauti.

Netanyahu, ambaye amekana makosa, atahitaji uungwaji mkono wa zaidi ya nusu ya wabunge kupewa kinga hiyo.

Kiongozi huyo wa muda mrefu wa nchi hiyo, alidaiwa kukubali kuchukua zawadi kutoka kwa wafanyabiashara matajiri na kutoa hongo ili aweze kuwa katika vyombo vya habari mara kwa mara.

Alitoa ombi hilo la kinga ya bunge kupitia hotuba ilipeperushwa kwenye televisheni saa nne kabla ya muda wa mwisho wa kutoa ombi hilo kumalizika.

Alisema: "Nafanya hivi kwa mujibu wa sheria, kwa lengo la kuendelea kuwahudumia na mustakabali wa siku zijazo Israel".

Mwezi Machi, atakabiliwa na uchaguzi wa tatu wa kitaifa katika kipindi cha mwaka mmoja. Kesi hiyo haiwezi kuanza hadi ombi la kinga litakapowasilishwa katika bunge la Israel, ambalo litakiwa kuvunjwa kabla ya uchaguzi, na huenda likatoa uamuzi kuhusu ombi hilo kabla ya hapo.

Chini ya sheria ya Israel, wanachama wa Knesset hawapewi kinga ya moja kwa moja dhidi ya mashtaka, lakini wanaweza kuomba kinga wakati hali ikiwalazimu kufanya hivyo. Waziri Mkuu wa Israel aliye madarakani anatakiwa kujiuzulu atakapo shtakiwa.

Chaguzi zilizopita zilizofanywa mwezi Aprili na Septemba mwaka 2019, chama cha Netanyahu cha mrengo wa kulia cha Likud kumekuwa katika njia panda dhidi ya Chama cha Blue na White, hivyo kusababisha kushindwa kuunda serikali.

Changamoto za kisheria zinazomkabili Netanyahu zimekuwa kizingiti katika yatapofanyika majadiliano. Amekuwa akisisitiza kuwa mashtaka hayo ni jaribio la mapinduzi dhidi yake.

"Sitakubali uongo kushamiri", alisema katika hotuba ya kupinga kesi hiyo.

Viongozi wa kisiasa nchini Israel wameghadhabishwa sana na uamuzi huo.

Hasimu Mkuu wa Netanyahu, Benny Gantz, ameapa kuwa chama chake cha Blue na White kitafanya kila liwezalo kuzuia kinga hiyo.

"Sijawahi kufikiria nitaona siku ambayo Waziri Mkuu wa Israel ataepuka mkondo wa sheria kwa kujaribu kuvuruga mchakato wa sheria," alisema.

Avigdor Lieberman, kiongozi wa mrengo wa kulia Yisrael Beiteinu, alitangaza Jumatano kuwa chama chake kitapiga kura dhidi ya ombi la kinga.

Spika wa Bunge, Yuli Edelstein, ambaye ni mwanachama wa Chama cha Netanyahu cha Likud, amesema atafanya mazungumzo kuhusu suala hilo wiki ijayo.

**BBC**




Waandamanaji wakishambulia jengo la ubalozi wa Marekani nchini Iraq juzi. **PICHA AFP**

# Pompeo afuta ghafla ziara barani Ulaya

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Mike Pompeo, ameahirisha ziara yake nchini Ukraine na mataifa mengine barani Asia, kufuatia shambulizi kwenye ubalozi wa Marekani mjini Baghdad.

Shambulio hilo linadaiwa kutekelezwa na watu wenye silaha wanaoungwa mkono na Iran.

Pompeo alitarajiwa kuwasili Ukraine siku ya Ijumaa katika ziara ambayo ingemfikisha pia Belarus, Kazakhstan, Uzbekistan na Cyprus.

Ofisi yake imesema Pompeo, atalazimika kubakia mjini Washington, kuendelea kufuatilia hali nchini Iraq ili kuhakikisha usalama na ulinzi wa raia wa Marekani kwenye kanda ya mashariki ya kati.

Siku ya Jumanne na Jumatano maelfu ya waandamanaji wanaoiunga mkono Iran, waliuzingira ubalozi wa Marekani mjini Baghdad na kuchoma moto baadhi ya maeneo na wengine wakijaribu kuparamia kuta za jengo hilo.

Waandamanaji hao walikuwa wakipinga shambulizi la wiki iliyopita lililofanywa na Marekani dhidi ya kundi la wanamgambo la Kataib Hezbollah.

## Papa aomba radhi kumchapa kibao muumini

**VATICAN CITY, Rome**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ameomba radhi kwa kitendo chake cha kumchapa kibao, mmoja wa waumini kwenye kanisa la St Peter's Square huko Rome.

Papa alikuwa akisalimiana na watoto na mahujaji, ghafla alishikwa mkono na mwanamke mmoja aliyekuwa kwenye umati wa watu waliokuwa karibu na alimvuta kwa nguvu karibu amwangushe.

Hali hiyo, ilimfanya Papa kugeuka na kumpiga makofi mawili mkononi mwanamke huyo kwa hasira.

Baadaye Papa alikiri kwamba alishindwa kujizuia na yeye pia huwa anakosea kama binadamu wengine.

Hivyo, anaomba radhi kwa kitendo hicho kwa muumini huyo na kila mtu.

Kitendo cha Papa cha kumzaba makofi ya mkononi mwanamke huyo, kimezua mjadala kwenye mitandao ya kijamii, hasa Twitter, wengi wakimuunga mkono Papa.

Awali wakati wa hotuba yake ya mwaka mpya, Papa alikemea unyanyasaji dhidi ya wanawake.

**BBC**

## Kiongozi wa upinzani ashinda urais Guinea Bissau

**GUINEA BISSAU, Bissau**

TUME ya uchaguzi nchini Guinea Bissau, imemtangaza kiongozi wa upinzani, Umaro Sissoco Embalo, kuwa mshindi wa uchaguzi nafasi ya urais.

Uchaguzi huo ulifanyika Desemba 29 na wa kwanza kuwa huru katika taifa hilo lenye hali tete la Afrika Magharibi.

Embalo, ambaye ni Jerenali wa Jeshi na Waziri Mkuu wa zamani ameshinda uchaguzi huo kwa kupata asilimia 53.6 ya kura dhidi ya asilimia 46.5 alizopata mpinzani wake.

Domingos Simoes Pereira, pia alikuwa Waziri Mkuu aligombea kwa tiketi ya chama tawala PAIGC.

Hata hivyo, Pereira amepinga matokeo hayo akisema uchaguzi huo ulikumbwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu na kwamba atawasilisha malalamiko mahakamani kupinga matokeo yake.

Embalo anachukua nafasi hiyo ya rais kutoka kwa Jose Mario Vaz, aliyeingia madarakani tangu 2014, kwa ahadi ya kutuliza mapinduzi ya mara kwa mara ya jeshi na mauaji tangu taifa hilo lilipopata uhuru wake kutoka kwa Ureno mwaka 1974.

**DW**

# LATRA yadhibiti ulanguzi nauli

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) mkoani Kilimanjaro, imeweka kambi ya siku kadhaa katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini ili kukabiliana na mawakala wa mabasi ya mikoani kuuza tiketi kwa bei ya 'kuruka'.

Jana, Nipashe lilishuhudia maofisa wa mamlaka hiyo wakiwa na gari dogo aina ya Toyota Pick Up ndani ya kituo hicho huku wakipita huku na huko kukagua tiketi na kuuliza maswali kwa baadhi ya abiria kama wameuziwa tiketi kinyume cha utaratibu.

Ofisa wa Latra aliyefahamika kwa jina moja la Masoud, alisema mamlaka inawakomalia wanaopandisha nauli mabasi ya mikoani na wanapambana na wanaopandisha nauli za mabasi kutoka Moshi kwenda Dar es Salaam na mikoa mingine ambao wanarejea baada ya kumalizika kwa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Inaelezwa kuwa maofisa hao wanafanya ukaguzi huo na kukamata mawakala wanaotoza nauli kubwa, kwa sababu yako malalamiko ya baadhi ya abiria kutozwa nauli kwa kiwango kisichokubalika.

Kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini hivi sasa kimefurika abiria wanaosafiri kwenda mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga kupitia Singida.

Baadhi ya abiria waliozungumza na Nipashe, walisema wanatozwa nauli kutoka Moshi kwenda Dar es Salaam hadi Sh. 35, 000 kwa mabasi ya kawaida wakati mabasi ya kisasa (Luxury) wanatozwa hadi Sh. 40,000.

Kwa sasa mji wa Moshi, umejaa idadi kubwa ya wageni wanaosafiri kwenda mikoa mbalimbali nchini, huku ukitishiwa pia na msongamano mkubwa wa magari madogo yanayotoka Moshi kwenda mikoani.

Msongamano huo ulitokana na utamaduni wa wenyeji wa mkoa wa Kilimanjaro, kurejea kwao kila inapofika sherehe za mwisho wa mwaka za Krismasi na Mwaka Mpya.

Jana, Nipashe ilishuhudia Mkuu wa Operesheni wa Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro, Peter Mizabwa, akiwa ameweka kambi katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi mjini akiwa na wakaguzi wengine wa Polisi kukabiliana na idadi hiyo ya wasafiri pamoja na ukaguzi wa mabasi hayo.

## Viongozi waonywa maslahi binafsi

**Na Dege Masoli, KOROGWE**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Korogwe, imewataka viongozi wa serikali za vitongoji na vijiji kutoitumia vibaya fursa waliyopewa ya mamlaka ya kutunga sheria ndogo kwenye maeneo yao kwa kupitisha zinazolenga maslahi binafsi hata kama ni kandamizi kwa wananchi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Mandia Kihiyo, alisema hayo jana wakati akifunga semina elekezi ya mafunzo maalum kwa viongozi wa serikali yaliyolenga kuwajengea uwezo katika utendaji wao.

Viongozi wanaoshiriki mafunzo hayo ni wa ngazi za vitongoji, vijiji na kata yenye lengo la kuwajengea uwezo na utambuzi wanapotekeleza majukumu yao kwa wananchi.

Kihiyo alisema serikali imewapa mamlaka ya kujitungia sheria ndogo na kwamba hiyo ni fursa, lakini alionya kuwa isitumike kama fimbo ya kuwaadhibu wananchi kwa kutunga sheria kandamizi na badala yake ziwe ni zenye maslahi mapana kwa jamii.

Aliwataka viongozi hao kuwa na uwazi katika mapato na matumizi ya fedha za serikali, kujenga ushirikishaji kwa wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo na kwamba kufanya hivyo kutawawezesha kufahamu kinachoendelea.

"Zingatieni hayo ndugu zangu ikiwa ni pamoja na kutoweka sheria ndogo ndogo zenye lengo la kuzitumia kwa ajili ya kuwakomoa wananchi na hatimaye kusababisha migogoro. Kufanya hivyo mtakuwa vyanzo vya migogoro," alisisitiza.

Kihiyo alisema kusudio la viongozi hao kupatiwa semina hiyo ni kuhakikisha wanasimamia kwa ukamilifu maelekezo yaliyomo kwenye miongozo ya majukumu yao kama vile kuitisha mikutano mikuu ya vijiji kwa mujibu wa katiba, kusoma mapato na matumizi katika maeneo yao na kwa wakati ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza na kuzorotesha maendeleo.

Naye Ofisa Tarafa ya Mombo, Alex Mhando, alisema matarajio yake baada ya mafunzo hayo ni kuleta tija kwa wananchi kutokana na ukweli kwamba viongozi hao ndio wanaoishi na wananchi wa ngazi ya chini ambao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha.

Mhando alisema kuwa ana imani kwamba baada ya kutambua wajibu na majukumu yao, watakwenda kuwa sehemu ya mabadiliko kuanzia ngazi ya jamii katika kushiriki kwenye miradi ya kijamii na maendeleo sambamba na kuleta mapinduzi ya kiuongozi.




Mkurugenzi Mkuu wa Swissport Tanzania, Mrisho Yassin (wa tatu kulia), pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mipango Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Kitula Yango ( wa tatu kushoto), wakikata keki wakati wakiingia makubaliano ya kufanya kazi pamoja kati ya Swissport na Air Tanzania, hafla hiyo iliyofanyika katika Viwanja vya Ndege Terminal 3 Dar es Salaam jana. Wengine p ni maofisa kutoka Swissport na ATCL. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wapewa ujuzi kutengeneza mifuko mbadala

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAJASIRIAMALI jijini Arusha wameamua kujifunza mafunzo ya muda mfupi ya utengenezaji mifuko mbadala ya karatasi kwa ajili ya vifungashio ili kukabiliana na upungufu wa mifuko utakaojitokeza.

Hatua hiyo inakuja baada ya serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

Wakizungumza jana katika hafla ya kuhitimu mafunzo ya wiki mbili ya kutengeneza vifungashio kwa kutumia karatasi, katika Chuo cha Ufundi cha Tanganyika Polytechnic, baadhi ya wahitimu hao waliishukuru serikali kwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo kwa kuwa imewawezesha kupata fursa ya kujifunza kuzalisha mifuko mbadala itakayowawezesha kujiajiri na kuongeza kipato.

Martha Mwakidebe, Rose Chisala na Neema Mgendi, walizungumza kwa niaba ya wenzao, waliipongeza serikali kwa hatua ya kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki.

Walisema wakiwa wajasiriamali wadogo, hatua hiyo imewapa fursa ya kujifunza na kuanzisha viwanda vidogo kwa ajili ya kuzalisha mifuko mbadala ambayo imeanza kuwanufaisha.

"Hii fursa itatusaidia sisi wajasiriamali kujiajiri kwa kutumia ujuzi tulioupata kutengeneza mifuko mbadala ili kupiga vita matumizi ya mifuko ya plastiki," alisema Rose Chisala.

Naye Meneja wa Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kufunga mafunzo hayo, aliwataka wahitimu kutumia fursa hiyo kuanzisha viwanda vidogo kwa ajili ya kuzalisha vifungashio.

Nchimbi alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wanaunga mkono sera ya serikali kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda.

Alikipongeza chuo hicho cha Tanganyika Polytechnic kwa ubunifu na kuanzisha mafunzo ya ufundi stadi yatakayowasaidia kuwajengea uwezo wa kufanya kazi za kuzalisha kupitia ujuzi walioupata.

Awali, Mkuu wa chuo hicho, Abdul Semvua, alisema mafunzo hayo ni ya tatu kuhitimu tangu waanzishe programu hiyo, ambayo imelenga kuunga mkono katazo la serikali kuhusu uzalishaji wa mifuko ya plastiki kwa kutoa elimu ya ujuzi kwa wajasiriamali kutengeneza mifuko ya karatasi.

"Tumekuwa na mafanikio makubwa tangu tuanzishe programu ya kutoa ujuzi kwa wajasiriamali kutengeneza mifuko ya makaratasi. Wengi waliohitimu kwa sasa wanatengeneza vifungashio na wameanza kuonja mafanikio," alisema Semvua.

Awali, mbunifu wa mitaala katika chuo hicho, Dk. Richard Masika, alisema nia ya chuo ni kujenga uwezo wa ujuzi kwa wajasiriamali ili wawe na uthubutu wa kuanzisha viwanda vidogo na kuondoa dhana iliyojengeka kwamba wenye uwezo wa kuanzisha viwanda ni wageni kutoka nje ya nchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

### LOSS OF CERTIFICATE



115571402

**NAZRINA SARFARAZ HASHMI** do here by announce the loss of Her Certificate of ALL INDIA SECONDARY SCHOOL EXAMINATION 2000 (ORIGINAL CERTIFICATE) which issued by INDIAN SCHOOL DAR ES SALAAM TANZANIA, 2000. Whoever finds it, kindly report to the nearest police station. REF NO: **DAR/MSI/RB/1180/2020.**

### PASSPORT IMEPOTEA



115571502

**BEATRICE INNOCENT KAMENGE** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB 10598759** Iliyotolewa mwaka 2017 Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/596812/2019.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN JOSEPH MAZAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 913 CAJ** aina ya **SUZUKI CARRY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/340/2020.**

115571702

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako*

*la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# POGBA
## ASHAURIWA KUFANYIWA OPERESHENI

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba ameshauriwa kufanyiwa operesheni ya enka, kwa mujibu wa kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer.

Solskjaer alitarajia Pogba kuwa fiti na kujiunga na kikosi cha United kwenye mchezo dhidi ya Arsenal juzi, lakini alibainisha kwamba, matatizo ya kifundo cha mguu yanayomsumbua kiungo huyo yanaweza kumfanya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Pogba alicheza wakati United ikifungwa 2-0 na Watford Desemba 22, mwaka jana na akaichezea United wakati ikiichapa Newcastle United mabao 4-1 siku ya 'Boxing Day'.

Baada ya kushuhudia kikosi chake kikifungwa 2-0 na Arsenal pale kwenye dimba la Emirates, Solskjaer aliulizwa anamtarajia Pogba kukaa nje kwa kipindi gani, na aliiambia BT Sport: "Sijui, wiki tatu au nne pengine.

"Ameshauriwa kufanyiwa operesheni na watu wake na pengine atafanya hivyo."

Solskjaer alifafanua kuhusu klabu kujihusisha na matibabu ya Pogba akiwaambia waandishi wa habari: "Alifanyiwa uchunguzi, hakuna kitu kikubwa sana, ni kitu ambacho kitafanyika ndani ya muda uliopangwa.

"Ameshauriwa kufanya hivyo haraka inavyowezekana, na pengine atafanya haraka zaidi. Tulikutana na washauri wanaomwangalia. Uchunguzi umefanywa na sisi."

United walifungwa kwa mabao ya Nicolas Pepe dakika ya nane na miamba hao wa Landon Kaskazini, na Arsenal ilifunga la pili kupitia kwa Sokratis Papastathopoulos kabla ya mapumziko.

## 'JESUS NI NOMA SANA, LAKINI AGUERO NOMA ZAIDI'

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amemsifia Gabriel Jesus baada ya kufunga mabao mawili dhidi ya Everton, lakini amemtaja Sergio Aguero kuwa "pengo lake halizibiki" pale Manchester City.

Mabao ya haraka ya Jesus mapema kipindi cha pili yaliwahakikishia City ushindi dhidi ya Toffees hao, ambao walipata bao la kufutia machozi kupitia kwa Richarlison baada ya makosa ya Claudio Bravo.

Wakati huo huo, Aguero, ambaye alirejea uwanjani baada ya kuwa majeruhi kwa muda mrefu wakati City wakipata ushindi wa 2-0 dhidi ya Sheffield United Jumapili iliyopita, alibakia kuwa benchi na hakutumika.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Jesus sasa amefikisha mabao 13 kwa jina lake katika mashindano yote msimu huu, lakini Guardiola amesisitiza Aguero bado namba moja.

"Gabriel ni mchezaji kwenye akili, lakini pengo la Sergio halizibiki," alisema Guardiola akinukuliwa na mtandano wa Twitter wa City.

"Ana maana kubwa kwetu na kwa mashabiki, kile alichokifanya dhidi ya QPR (mwaka 2012), tunahitaji wachezaji wote, lakini Sergio amempa zawadi Gabriel.

"Wana mahusiano mazuri. Na hilo ndio linalochangia kucheza vizuri na kwa kujituma zaidi kwa kikosi hicho."




## NEYMAR AANDAA MIKAKATI KURUDI BARCELONA

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameripotiwa anaandaa mikakati maalumu kuhusu ofa yake ya kurudi kwenye klabu yake ya zamani ya Barcelona.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi tena Camp Nou katika kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini akaishia kubakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Hata hivyo, Neymar bado anaonekana kwamba anaangalia uwezekano wa kurudi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Neymar sasa anaandaa mikakati rasmi ya kurudi Barcelona, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anataka kuhama na kulitaka Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kuweka wazi fidia ambayo atatakiwa kuilipa PSG ili wamwachie, kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Neymar amefunga mabao tisa katika mechi 12 msimu huu, akiwa anasumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara.






# SOLSKJAER: TUTASAJILI MMOJA AU WAWILI

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amedokeza kuhusu usajili wa Januari wa Manchester United, akisema kwamba klabu hiyo ya Ligi Kuu England "itaangalia nyota mpya mmoja au wawili" kwa ajili ya kuongeza nguvu.

United ilifungwa mabao 2-0 na Arsenal Jumatano, na kuachwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu na ikipitwa pointi tano na wanaoshika nafasi ya nne Chelsea.

Eneo la kiungo ya kati ndio lilionekana kuwa na tatizo kubwa pale United, huku Paul Pogba akisumbuliwa na enka na Scott McTominay (goti) na kuwafanya kukaa nje kwa wiki kadhaa.

Solskjaer amesema kwamba atataka kufanya usajili, lakini akaongeza ni kama tu United itaweza kutafuta mchezaji sahihi.

"Unaweza kuona kikosi chetu na wakati mwingine ukafikiria kuhusu kuongeza mmoja au wawili," alisema.

"Inategemea na namna tutakavyofikiri na kuona nani yupo kwa ajili yetu. Bila shaka tunataka angalau wachezaji wawili, Scott atakuwa nje kwa miezi miwili na Paul kwa mwezi mmoja.

"Hilo litatupa sisi chaguo na tunatakiwa kuangalia kwenye mechi muhimu tu zilizopo mbele yetu.

"Lakini tutaangalia mchezaji sahihi na sio yoyote, kwa sababu tunamhitaji yule atakayekuwa msaada kwenye kikosi chetu."

## Guardiola: City walipambana vizuri kwa Everton

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola alisifia morali ya kikosi cha Manchester City kwa ushindi wao dhidi ya Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England hapo juzi.

Mabao mawili ya Gabriel Jesus ya kipindi cha pili yaliiwezesha City kupata ushindi wa 2-1 nyumbani na kukifanya kikosi hicho cha Guardiola kilichopo nafasi ya tatu kupunguza tofauti ya pointi hadi 11 dhidi ya vinara Liverpool, ambao wamecheza mechi chache zaidi.


Kocha huyo wa City alisema aliridhishwa na kiwango cha timu yake, wakati kikiendelea kuimarika kwenye kupambana katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu licha ya kupitwa pointi nyingi na Liverpool.

"Tulicheza vizuri. Nimehamasika na kiwango cha timu, wachezaji walionyesha ari nzuri na morali ya juu," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Kuwa mbali baada ya kuwa mabingwa kwa misimu miwili, timu ikiwa kwenye hali nzuri, unaweza kukata tamaa.

"Pengine tutamaliza nafasi ya saba au nane kwenye msimamo, lakini kwa sababu hatujaribu. Mechi ziko pale na tulicheza vizuri, na tukapata ushindi mzuri."

Guardiola aliamua kutumia mfumo wa 3-4-3 dhidi ya Everton, akiwaanzisha Eric Garcia, Fernandinho na Rodri kwenye safu ya ulinzi, huku Benjamin Mendy na Joao Cancelo wakicheza pembeni.



## Xhaka haondoki Arsenal – Arteta

**LONDON, England**

GRANIT Xhaka amemhakikishia Mikel Arteta kwamba atabakia katika klabu ya Arsenal, kwa mujibu wa kocha huyo.

Xhaka aliripotiwa kufikia makubaliano ya kujiunga na klabu ya Hertha Berlin wakati huu wa dirisha dogo la usajili, huku majaliwa yake pale Arsenal yakiwa shakani tangu alipokwaruzana na mashabiki wakati wakitoka sare ya 2-2 na Crystal Palace Oktoba mwaka jana.

Lakini baada ya kuukosa mchezo wa Arsenal waliopoteza 2-1 kwa Chelsea Desemba 29, Xhaka alianza mwaka 2020 vizuri baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Manchester United.

Alipoulizwa kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amemhakikishia kama atabakia kwenye dimba hilo la Emirates, Arteta aliwaambia waandishi wa habari: "Ndio, amenihakikishia.

"Nafikiri atabakia na sisi. Kwa uhakika nampenda. Kama akibakia kwenye kikosi chetu, atakuwa mchezaji muhimu zaidi kwetu."

Mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Nicolas Pepe na Sokratis Papastathopoulos yalikisaidia kikosi hicho cha Arteta kupata ushindi wake wa kwanza tangu akichukua nafasi ya kuwa kocha wa Arsenal na alikisifia kikosi chake kwa kiwango bora.

Arteta alibainisha kwamba kuna mengi yanakuja kutoka kwa wachezaji wake hao, ambao alisema bado hawajafiti.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LUIZ AITABIRIA MAZURI ARSENAL

Beki huyo asema chini ya Arerta kikosi chao kina uwezo wa kufanya mambo makubwa...

**LONDON, England**

BAADA ya kufanikiwa kuifunga Manchester United, beki wa Arsenal, David Luiz, amesema kuwa timu yake ina uwezo wa "kufanya mambo makubwa" ikiwa chini ya kocha mpya, Mikel Arteta.

Sokratis Papastathopoulos na Nicolas Pepe walifunga katika ushindi wa mabao 2-0 ambao uliifanya Arsenal kupaa hadi katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi nne nyuma ya United iliyoko katika nafasi ya tano.

Ilimaliza wakati mbaya wa kucheza mechi saba bila ya kupata ushindi kwenye uwanja wa nyumbani, tena ukiwa ushindi wa kwanza dhidi ya timu zilizoko kwenye nafasi 10 Bora kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Ninaamini chini yake (Arteta), kila mchezaji ataimarika," alisema Luiz ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 32.

"Mikel ni kocha mkubwa na anayeufahamu vema mpira wa miguu. Ni mchezaji mkubwa, anatuletea vitu vipya na ninaamini katika filosofia yake.

"Tunatarajia kufanya mambo makubwa ndani ya muda mfupi ujao, lakini tutaenda hatua kwa hatua."

Baada ya kupata sare mara mbili na kufungwa mchezo mmoja kocha huyo mwenye umri wa miaka 37 ambaye alikuwa akiinoa Manchester City, Arteta alitua klabuni hapo ili kuokoa jahazi lililokuwa linaelekea pabaya la timu hiyo inayotumia Uwanja wa Emirates.

Ingawa Manchester United haikuwa na bahati katika mechi hiyo, The Gunners walikuwa bora zaidi katika kipindi cha kwanza na Pepe alifanikiwa kuisumbua safu ya ulinzi ya wapinzani wao.

Lakini kulikuwa na kiwango bora katika upande wa kiungo kilichoongozwa na Mesut Ozil, ambaye alifanikiwa kutawala eneo kubwa na kuwachezesha wachezaji wote wa Arsenal, Lucas Torreira alikimbia kilomita 11.54 na Granit Xhaka, ambao Arteta anahitaji kuona wanabakia klabuni hapo licha ya kuhusishwa na tetesi za kuelekea Hertha Berlin.

Luiz aliiambia BT Sport: "Tulicheza vizuri sana katika kipindi cha kwanza, na tulionyesha ukomavu kwenye kipindi cha pili. Tunatakiwa pia kuwa wakweli na kukubali kwamba hatukuwa vema katika 'fiziki' na hatukuwa tayari. Lakini unapokuwa hauko fiti unatakiwa kupambana na kuuweka moyo wako tayari.

"Huwezi kubadilisha kutoka sifuri mpaka namba 10 kwa siku moja, wiki moja, mwezi mmoja, lakini ni vizuri kuona kuwa hawa vijana wameanza kuelewa na kufanya majukumu yao, namna wanavyojipanga kuhakikisha wanafanya mambo makubwa na vitu vikubwa kwenye mpira.

"Katika maisha unapokuwa na furaha, matokeo yanakuwa tofauti. Kama ulilala na furaha, unaweza kulala kwa saa nne vizuri kuliko ukiwa na huzuni na ukalala saa nane ambazo hazina maana. Kama utafanya kazi ukiwa na furaha na unaamini kile unachokifanya unaweza kuzalisha mambo tofauti.

"Msimu huu si msimu wetu. Tulianza vibaya sana, lakini mambo yameanza kubadilika na bado tuna nafasi ya kupambana kuwania mataji mengine na hii itatuimarisha kuelekea msimu unaokuja."

## KWA UFUPI

**JUVENTUS YAMTAKA POGBA**

JUVENTUS inajipanga kuanza mchakato wa kumrejesha kiungo wake wa zamani, Paul Pogba (26), kutoka Manchester United kutokana na sintofahamu aliyonayo kwenye maisha ya kikosi cha Old Trafford. ***(Calciomercato)***

**UNITED, RB WAJIPANGA**

MANCHESTER United inataka kutengeneza mazingira ya kumnasa straika wa RB Leipzig, Timo Werner (23), kwa kukamilisha makubaliano na vinara hao wa Bundesliga, lakini wakiruhusu nyota huyo aendelee kubakia klabuni hapo hadi mwisho wa msimu. ***(Express)***

**NAPOLI, AJAX VITANI**

NAPOLI na Ajax zimeweka wazi nia ya kumwania beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen, kwa kuitaka klabu yake ya Tottenham ikubali kumuuza katika dirisha dogo la usajili la Januari kabla ya kusubiri nyota huyo aondoke kama mchezaji huru kwenye majira ya kiangazi. ***(Telegraph)***

**MANE ANUKIA LIVERPOOL**

REAL Madrid imeanza mazungumzo na wakala wa straika wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Senegal, Sadio Mane, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Le10Sport)***

**STURRIDGE AINGIA SOKONI**

KLABU za Marseille na Aston Villa ni baadhi ya timu zinazowania saini ya straika wa zamani wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Daniel Sturridge (30), ambaye kwa sasa anaitumikia klabu ya Trabzonspor ya Uturuki. ***(Mail)***

**FERGUSON AKARIBIA SPURS**

TOTTENHAM inaongoza katika mbio za kuwania saini ya beki wa West Brom, Nathan Ferguson, ambaye klabu yake maarufu kwa jina la Baggies inalazimika kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 ambaye anawindwa na Crystal Palace. ***(Mirror)***

**ERIKSEN BADO AGOMBEWA**

INTER Milan imejiunga katika vita ya kuwania saini ya kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 anatarajia kuwania mkataba wake na klabu hiyo katika kipindi cha majira ya joto na pia anawaniwa na Manchester United, Paris St-Germain na Juventus. ***(Mail)***

**SOUMARE MAMBO SAFI**

MANCHESTER United na Tottenham zitachuana kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Lille, Boubakary Soumare. Inaelezwa kuwa klabu sita zimewasilisha ofa ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

**XHAKA AMSUBIRI ARTETA**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Uswisi, Granit Xhaka (27), anatakiwa kusubiri kujua hatima yake kutoka kwa Kocha mpya wa Arsenal, Mikel Arteta, kuhusu ombi lake la kutaka kujiunga na Hertha Berlin katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa. ***(Independent)***

**LAMPARD AGHAIRI KWA ZAHA**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesitisha uamuzi wa kumwania mshambuliaji wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha (27), katika kipindi cha usajili cha dirisha dogo la Januari. ***(Star)***

**LALLANA KUONDOKA LIVERPOOL**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kuwa kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Adam Lallana (31), anaweza kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu ambapo mkataba wake utakuwa umemalizika. ***(Mirror)***

**FERNANDES AITAJA SPURS**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ureno na Sporting Lisbon, Bruno Fernandes (25), ambaye aliwahi kuwania na Manchester United, amesema kuwa anakaribia kujiunga na Tottenham katika kipindi cha majira ya joto kuliko timu nyingine. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# MGOSI AFUNGUKA MECHI YA WATANI ISIVYOTABIRIKA

Na Shufaa Lyimo

ALIYEKUWA mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema kuwa wachezaji wa timu hiyo wanatakiwa kuongeza umakini kuelekea mechi dhidi ya watani zao Yanga kwa sababu mchezo huo huwa hautabiriki.

Simba inatarajia kuwakaribisha Yanga katika mechi ya kwanza ya msimu huu, itakayochezwa kesho Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgosi, ambaye sasa ni Kocha Mkuu wa Simba Queens, alisema kuwa Simba inauwezo wa kuwafunga watani zao, lakini watafanikiwa hilo tu endapo wataongeza bidii.

Mgosi alisema kuwa Simba ina wachezaji wenye viwango vizuri ukilinganisha na watani zao, hivyo anaamini wana nafasi nzuri ya kuondoka na pointi tatu.

"Simba inauwezekano wa kushinda kwa sababu haijasajili wachezaji wapya, wanatarajia kutumia nyota wale wale waliozoeana katika mchezo huo, tofauti na Yanga ambao wamesajili wachezaji wengi, ambao mpaka sasa bado hawajajuana vizuri," alisema Mgosi.

Aliongeza kuwa mchezo unatarajiwa kuwa wa kuvutia kutokana na 'majigambo' yanayoendelea kutolewa na makocha, viongozi, mashabiki na wanachama wa timu hizo zote za jijini.

Aliwataka mashabiki wa Simba wajitokeze kwa wingi uwanjani kuishangilia timu yao ambayo mpaka sasa inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo inashirikisha timu 20.

"Ni mechi ambayo kila mchezaji anahitaji kupata nafasi, ni mechi inayowatengeneza nyota wapya na inayowapoteza wengine, ni mchezo ambao huwa hautabiriki, ila kwa mimi nina imani na kikosi chetu," Mgosi alisema.

Simba itashuka uwanjani kesho ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ndanda FC, wakati Yanga wao walipata bao la 'jioni' ilipowakaribisha Biashara United kutoka Musoma, mkoani Mara.

Vinara hao wa Ligi Kuu pia wanakumbukumbu ya kupata ushindi wa mabao 6-0 katika mechi yao ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Arusha FC, wakati Yanga ilipata ushindi wa magoli 4-0 dhidi ya Iringa United, katika michuano hiyo.



Mshambuliaji wa Manchester City, Kevin De Bruyne (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Everton, Fabian Delph, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku.City ilishinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Mziba akabidhiwa majukumu Yanga

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Yanga umemtangaza, Abeid Mziba, kuwa Kaimu Meneja wa timu hiyo akichukua nafasi iliyoachwa na Dismas Ten, ambaye amesimamishwa kwa muda usiojulikana, imeelezwa.

Ten alisimamishwa na uongozi wa klabu hiyo kwa tuhuma za kuruhusu benchi la ufundi la Yanga kuvaa jezi 'feki' katika mechi dhidi ya Biashara United, ambayo ilichezwa mapema wiki hii.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Yanga, David Luhago, alisema kuwa uteuzi wa Mziba umefanywa kwa kuzingatia uwezo na weledi alionao wa kuitumikia vizuri nafasi hiyo.

Luhago alisema kuwa tayari Mziba, ambaye mwaka jana alikuwa ni Meneja wa Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), iliyoshiriki Kombe la Chalenji jijini Kampala, Uganda, ameshaanza majukumu yake mapya na anaamini atakuwa na wakati mzuri.

"Uongozi umeamua kumpa Mziba jukumu hili baada ya Dismas kupewa jukumu lingine," alisema Luhago.

Kuelekea mechi yao dhidi ya Simba, kiongozi huyo alisema kuwa maandalizi ya kikosi chao yamekamilika na wanawaomba wanachama na mashabiki wao wajitokeze kwa wingi kuishangilia timu.

Wakati huo huo, mashabiki wa klabu hiyo waliokuwa wanasafiri wa kutumia baiskeli kutoka mkoani Mtwara waliwasili salama jijini jana.

Luhago alisema kuwa kutokana na kutambua mapenzi yao kwa klabu, uongozi wa Yanga umeamua kuwapa huduma ya malazi kwa siku mbili pamoja na tiketi za bure kushuhudia mchezo huo.

# Namungo kusajili wachezaji wanne

Na Mwandishi Wetu

KATIKA kuhakikisha kikosi chao kinakuwa imara na kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa timu ya Namungo FC ya mkoani Lindi umesema unatarajia kusajili wachezaji wapya wanne katika kipindi cha dirisha dogo.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilifungua rasmi dirisha dogo la usajili wa wachezaji tangu Desemba 15, mwaka jana na linafunga mchakato huo ifikapo Januari 15, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, aliliambia gazeti hili kuwa wanahitaji nyota wapya wanne ili wafanye vizuri katika hatua ya lala salama ya ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Zidadu alisema kuwa tayari wameshaanza mazungumzo na nyota mbalimbali na anaamini mchakato huo utakapokamilika, kikosi chao kitapata nguvu mpya.

"Timu imesharudi Lindi kujiandaa na mchezo wetu wa Ijumaa, lakini mimi nimebaki Dar es Salaam ili kukamilisha masuala ya usajili, siwezi kusema nani tutamsajili, tuko katika mazungumzo na yatakapokamilika tutaweza wazi, ila tunadhamiria kusajili wachezaji wanne," alisema Zidadu.

Aliongeza kuwa kati ya wachezaji hao wapya, washambuliaji watakuwa wawili na hayo ni mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi la timu hiyo.

"Bado tuko kwenye malengo yetu, wakati tumepanda daraja na msimu huu ulipoanza, tuliweka malengo yetu kwamba tunahitaji kubakia kwenye Ligi Kuu, tunashukuru hili kwa nafasi tuliyopo, lakini tutahitaji kuimarika na kufanya vizuri zaidi," Zidadu alisema.

Namungo FC yenye pointi 22, imecheza mechi 13 na katika msimamo wa Ligi Kuu Bara iko katika nafasi ya sita wakati Singida United ambao wamejikusanyia pointi saba na iliyoshuka dimbani mara 14, inaburuza mkia.


Kikosi hicho cha Namungo kinaendelea kujinoa kwa ajili ya kuwafuata wapinzani wao Mbeya City katika mechi ya raundi ya 15 ya ligi hiyo inayotarajiwa kuchezwa Januari 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani Iringa.

Michezo
Ijumaa Januari 3, 2020
Nipashe



## Luiz aitabiria mazuri Arsenal

HABARI UK 30




Kipa wa Manchester United, David de Gea, akiruka kuwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette (kushoto), katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAFUNGUKA ILIPOWAZIDI YANGA

●●●Lakini Manara atahadharisha lolote linaweza kutokea katika mechi za watani...

**Na Somoe Ng'itu**

JOTO la pambano la watani wa jadi nchini, Simba na Yanga limeendelea kupanda huku msemaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Haji Manara, akitamba kuwa anaamini kwa asilimia kubwa Wekundu wa Msimbazi, wataibuka na ushindi katika mchezo wa kesho.

Hata hivyo, Manara, alisema kuwa katika soka na hasa kwenye mechi za watani wa jadi, lolote linaweza kutokea.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Manara, alisema kuwa sababu namba kuu inayowapa 'jeuri' ni ubora wa kiufundi uliopo katika kikosi chao.

Manara alisema kuwa haoni sababu ambayo inaweza kuikosesha ushindi timu yake na kwa maandalizi mazuri waliyofanya wachezaji wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema pia kikosi cha Simba kina wachezaji wenye uzoefu zaidi ukilinganisha na nyota walioko katika kikosi cha wapinzani wao ambao kwa sasa wanafundishwa na Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa.

"Kiufundi... hakuna namna ya Yanga kushinda, ama kupata sare, achana na 'dabi' achana na mazingira, hesabu mmoja mmoja, juzi kuna mchambuzi ambaye anaheshimika, alimweka mchezaji mmoja tu anaweza kucheza katika kikosi cha Simba, alimtaja Kelvini (Yondani), na mimi siamini kama anaweza kucheza, atamweka nani nje, Erasto (Nyoni) akae nje, Wawa akae (Paschal)," alisema Manara.

Aliongeza kuwa hawezi kusema kuwa wanakwenda kufungwa na Yanga, huo ndio utamaduni wa kawaida wa mechi za 'dabi'.

"Ndio utamaduni wa 'dabi' zilivyo, hatuendi kusema tunaenda kufungwa na Yanga, nazungumzia kiufundi, sio nje ya uwanja, katika hali ya kawaida, simjui mshabiki hata mmoja, nchi nzima, hayupo, anayeweza kuamini timu yake inakwenda kumfunga Simba," Manara alisema.

Aliongeza kuwa anaamini Mkwasa ni mzoefu na mechi hizo za watani, kikosi chao kitaibuka na ushindi mnono katika mchezo huo.

"Siamini kama atakuja na mbinu nyingine yoyote zaidi ya 'kupaki basi', kama yuko makini, la sivyo, anataka kufunguka, na tutampiga tano, akifunguka na kutaka kucheza 'open game', Wallah tutampiga mkono," Manara alisisitiza.

BOCCO YUKO KAMILI...

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili kuwa hatima ya nahodha wa timu hiyo, John Bocco, kuanza katika kikosi cha kwanza katika mchezo wa kesho itajulikana kesho asubuhi.

Matola alisema kuwa kiafya, ameshapona na uzoefu alionao katika mechi zenye ushindani, unaweza kumpa nafasi ya kuanzia kwenye mchezo huo ambao utachezeshwa na refa, Jonesia Rukyaa, kutoka Bukoba, mkoani Kagera.

## Niyonzima atua, aahidi makubwa

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa kimataifa wa Yanga, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, amesema kuwa yuko tayari kwa mchezo wa kesho dhidi ya watani zao Simba, lakini akiomba ushirikiano kutoka kwa wachezaji wenzake.

Niyonzima alitua nchini jana mchana kwa ajili ya kurejea kwa mara ya pili katika klabu yake hiyo akitokea AS Kigali ya nchini kwao Rwanda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Niyonzima, alisema kuwa amekuja nchini kwa kazi moja ya kuisaidia Yanga iweze kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba, alisema kuwa anahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wachezaji wenzake ili watimize malengo ya timu hiyo iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

"Peke yangu siwezi kufanya lolote, ninahitaji ushirikiano, ninaamini kwa pamoja tutafanya kizuri," alisema Niyonzima.

Kuhusu mechi ya kesho dhidi ya Simba, Niyonzima, alisema kuwa yuko tayari kwa mchezo huo na endapo akipata nafasi ya kucheza hapo kesho, ataitendea haki fursa hiyo.

"Niko vizuri, nilikuwa nafanya mazoezi, ni mechi kubwa, ina mambo mengi, nimecheza sana hizo mechi, ni mechi ninayoiheshimu, sisi kama wachezaji kikubwa tunatakiwa kujiandaa kisaikolojia, napenda kuwaambia Wana-Yanga nimekuja kufanya kazi," alisema Niyonzima.

Aliongeza kuwa Tanzania ni nyumbani na kukubali kurejea ni ishara kamili kwamba yuko tayari kufanya kazi kwa kiwango cha juu.

Niyonzima alikuwa mmoja wa nyota walioisaidia Simba kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, lakini aliachwa na aliyekuwa Kocha Mkuu, Patrick Aussems.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >